

Mwongozo kuhusu

# Nyenzo za uwajibikaji wa kijamii

## Jinsi ya kujumuisha utetezi katika mchakato wa CCT

tearfund

## Je, lengo la mwongozo huu ni nini?

**Hii ni nyenzo ya kina inayoangazia vigezo muhimu vya uwajibikaji wa kijamii ili kuhusisha utetezi katika mchakato wa CCT.**

## Mwongozo huu unalenga nani?

Waelekezi, viongozi wa kanisa, na watetezi wanaohusika katika ustawi wa kanisa na jamii wanaweza kutumia nyenzo hizi kudumisha uwazi na uongozi bora, navyo vitengo vya usimamizi vinaweza kutumia nyenzo hizi katika kuboresha utoaji huduma.

Kila nyenzo ina maelekezo mahususi kuhusu jinsi ya kuitumia, na jinsi ya kuhakikisha utaratibu unaambatana na muktadha husika.

**Waandishi**
Chalwe Mumba Nyirenda na Kathleen Needham



tearfund

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 4 |
| Uwajibikaji wa kijamii unahusu nini? | 6 |
| Marejeleo ya Biblia kuhusu uwajibikaji wa kijamii | 7 |
| Malengo makuu ya nyenzo za uwajibikaji wa kijamii | 11 |
| Jinsi ya kutumia nyenzo hizi | 13 |
| Nyenzo ya mchakato wa mipango shirikishi | 17 |
| Nyenzo ya ufuatiliaji wa bajeti | 43 |
| Nyenzo ya uandishi wa habari wa raia | 72 |
| Nyenzo ya kadi ya tathmini ya jamii | 91 |
| Nyenzo ya uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma | 116 |
| Nyenzo ya ukaguzi wa kijamii | 136 |
| Kiambatisho: Hatua muhimu za mpango wa maendeleo ya serikali | 159 |
| Marejeleo | 161 |

# Utangulizi

Tearfund inaamini kuwa makanisa ya kieneo – kote duniani – huanza safari ya kudumu wanapokubali na kujitolea kufuata theolojia ya kile tunachokiita ‘utume wa kuishi maisha kikamilifu’. Safari hii huwatia nguvu, hubadili mawazo na huleta mabadiliko kamili kwenye kanisa na jamii.

Lengo kuu la safari hii ni kurejesha mahusiano yaliyovunjika. Kanisa linapaswa kuazimia kubadili 'maisha kikamilifu’, na kushughulikia kwa kina mahitaji ya jamii husika. Juhudi za kukabiliana na umaskini katika jamii zinachukuliwa kwa upana na zinahusisha wanajamii wenyewe, kadri wanavyozidi kutambua vipaji na rasilimali ambazo Mungu amewapa. Hatima ya safari hiyo ni 'ustawi wa kanisa na jamii' (CCT).[1]

Tunaamini kwamba kuhusisha utetezi katika mchakato wa CCT huimarisha matokeo na bila shaka huchangia katika maono ya kubadili ‘maisha kikamilifu’. Mbinu hii hutumia mikakati na hatua za utetezi zinazochangia uongozi bora na kuwezesha serikali mbalimbali kutoa huduma kwa uwazi na kwa njia inayofaa.[2] Juhudi za kutetea ustawi wa kanisa na jamii zinahusisha utetezi huu katika mchakato wa CCT kupitia nyenzo za uwajibikaji wa kijamii.

[1]Masuala ya kimsingi kuhusu ustawi wa kanisa na jamii (CCT) - Tearfund Learn

[2]Lawson na Watson (2016)

Mwongozo huu wa uwajibikaji wa kijamii unakusidiwa kuwa nyenzo ya kina inayoangazia vigezo muhimu vya uwajibikaji wa kijamii vya kutumiwa hasa na waelekezi wa utetezi wa CCT (wafanyakazi wa Tearfund, viongozi wa kanisa, wakufunzi na waelekezi) ili kujumuisha utetezi katika juhudi zao za CCT. Pia unaweza kutumiwa na wahusika wote wa utetezi wenye nia ya kujenga uwezo wa wanajamii ili kuwawezesha kuongoza juhudi za utetezi katika jamii zao.

Kama mtumiaji wa mwongozo huu, tungependa kujua kile ambacho umejifunza. Wasiliana nasi ikiwa unahitaji usaidizi wowote. Unaweza kuwasiliana nasi kupitia publications@tearfund.org.

Ili unufaike zaidi kutokana na nyenzo hii, rejelea pia:

- **Mwongozo wa utetezi** wa Tearfund
- **Nyenzo kuhusu utetezi katika karne ya kidijitali**
- **Mwongozo wa utetezi wa CCM**

Kila mwongozo unapatikana pia kwa Kifaransa, Kireno na Kihispania.

# Uwajibikaji wa kijamii unahusu nini?

**Uwajibikaji wa kijamii ni 'kiwango na uwezo wa wanajamii kuifuatilia serikali na watoa huduma ili kuwashinikiza wawajibike na washughulikie mahitaji ya wananchi na wanaopokea huduma'.[3]**

Hivyo, raia, jamii, kanisa, vyombo huru vya habari, na mashirika mengine yanaweza kutumia nyenzo za uwajibikaji wa kijamii kushawishi utoaji wa huduma bora, kwa kuwafanya watoa huduma wawajibike kama vile maafisa wa umma na watumishi wa umma. Mbinu za uwajibikaji wa kijamii zinaweza kutumika katika ngazi za kieneo na kitaifa na zinaweza kulenga masuala na michakato mbalimbali ya uongozi, ikiwemo:

- utoaji wa taarifa kwa umma, utungaji sera, uchanganuzi
- na ufuatiliaji wa bajeti za umma, matumizi ya fedha na taratibu za ununuzi
- ufuatiliaji unaoshirikisha wanajamii, na tathmini kuhusu utoaji huduma kwa umma
- majukumu makubwa ya usimamizi, hatua za kupambana na ufisadi na taratibu za kushughu likia malalamiko

**Lengo la uwajibikaji wa kijamii si kufutilia mbali taratibu za uwajibikaji zilizopo, bali ni kuimarisha na kuendeleza michakato hiyo.**

---

[3]Grandvoinnet, H. na wenzake.(2015). Opening the black box: The contextual drivers of social accountability

# Marejeleo ya Biblia kuhusu uwajibikaji wa kijamii



**Kuchambua Biblia Pamoja.** Picha: Aaron Koch/Tearfund

Tunamtumikia Mungu wa haki. Kama Wakristo, tunatakiwa pia ‘kutenda haki’ (Mika 6:8). Tafsiri ya Crossway ESV Study Bible inasema hivi:

> ‘Waabudu wa kweli wa Mungu watadhihirisha haki na utakatifu. Haki inazidi usawa wa kisheria; inarejelea ukamilifu wa utawala wa Mungu katika ulimwengu wake. Hivyo, upande wa serikali, "kutenda haki" kunamaanisha kutumia mamlaka kwa haki na usawa na kudumisha haki

> mahakamani, hasa katika kuwalinda wanyonge dhidi ya wenye nguvu. Upande wa mtu binafsi, "haki" inahusu kuendesha shughuli za biashara kwa haki na uaminifu, kuwa mwenye kusema ukweli, na pia kutowatumia vibaya maskini au wale wasio na hadhi au wenye udhaifu.'[4]

Hivyo, kutenda haki pia kunahitaji uwajibikaji; yaani, kunahitaji watu kuwajibika katika kutekeleza wajibu na majukumu yao kwa wengine. Simulizi moja kwenye Biblia kuhusu uwajibikaji linapatikana kwenye kitabu cha Ezra 8:28-34. Uchanganuzi wa Biblia katika jarida la Footsteps la Tearfund [5]unaangazia vigezo vitatu muhimu kuhusu uwajibikaji kama ilivyodhihirishwa na wanaume 12 katika kifungu hiki:

- uwajibikaji kwa Mungu
- uwajibikaji kwako binafsi
- uwajibikaji kwa wengine

Inasisitiza kwamba 'uwajibikaji wa kibiblia huanza kwa mtu kuwajibikia matendo yake na kumruhusu Mungu pamoja na watu wengine kumsaidia katika kutimiza yanayofaa.'[6]

Utetezi huhimiza uwajibikaji wa pande zote kati ya mtu na mwingine, kama ilivyo kwa serikali.

---

[4]Makala ya Crossway

[5]Uwajibikaji: Footsteps 76 (2008) – https://learn.tearfund.org/en/resources/footsteps/footsteps-71-80/footsteps-76

[6]David (2008) uk.11

*Mwongozo wa utetezi* wa Tearfund[7] unabainisha kuwa kwa Wakristo, utetezi ni ishara ya kumtii Mungu, ni tamanio la kuonyesha huruma na haki kwa wengine (hasa watu maskini, waliotengwa au walio katika mazingira magumu) na ni njia ya kuwaelekeza watu kwa Yesu Kristo. Mungu amewaweka Wakristo katika sehemu nyingi tofauti za kazi na kwenye jamii, na sehemu zote hizo zinahitaji kubadilika na kuimarika ili kukabiliana na umaskini. Wakristo wanahitaji kutumia ushawishi wao madhubuti kwa kufuata mfano kwenye Biblia:

- Kukataa dhuluma na ibada ya sanamu
- Kuwa kielelezo, kudhihirisha jinsi Mungu alivyokusudia jamii iwe
- Kukosoa viongozi wanapokwenda kinyume na mafundisho ya Biblia
- Kumwomba Mungu aingilie kati
- Kuleta amani na upatanisho
- Kutetea haki ya kijamii na kiuchumi

Nyenzo za uwajibikaji wa kijamii husaidia makanisa ya kieneo kufikia malengo haya, kwa kushirikiana na jamii.

---

[7]Soma kuhusu *Umuhimu wa utetezi*: *Marejeleo ya Biblia*, kwenye Mwongozo wa utetezi wa Tearfund, sehemu ya B3, kwa maelezo zaidi.

## Vifungu vya Biblia

- **Mithali 31:8-9 (NIV)**
  ‘Watetee wale wasioweza kujitetea, kwa ajili ya haki za wote walio wanyonge. Nena na uhukumu kwa haki; tetea haki za maskini na wahitaji.
- **Yeremia 22:3 (NIV)**
  ‘Hili ndilo asema BWANA: "Tenda yaliyo ya haki na sawa. Mwokoe mkononi mwa mkandamizaji, yule aliyekandamizwa. Msimtendee wovu mgeni, yatima au mjane, wala msimwage damu isiyo na hatia mahali hapa.”’
- **Kumbukumbu la Torati 25:13-16 (ESV)**
  ‘'Usiwe na vipimo hivi viwili mfukoni mwako, kubwa na ndogo. Usiwe na vipimo hivi viwili nyumbani mwako, kubwa na ndogo. Utakuwa na kipimo kamili na cha haki, naam, kipimo kamili na cha haki, ili siku zako ziwe nyingi katika nchi akupayo Bwana Mungu wako. Kwa maana wote wafanyao hayo, wote watendao kwa udanganyifu ni chukizo mbele za Bwana Mungu wako.
- **Zaburi 82:3 (NIV)**
  ‘Wateteeni wanyonge na yatima; walinde maskini na wanaoonewa.’

# Malengo makuu ya nyenzo za uwajibikaji wa kijamii

Mwongozo kuhusu *Uwajibikaji wa Kijamii*[8] wake Kohli unatoa muhtasari mzuri kuhusu malengo makuu ya nyenzo za uwajibikaji wa kijamii:

1. Kuwawezesha wananchi kushirikiana moja kwa moja na taasisi za serikali - kuchangia katika sera na kufuatilia utendakazi.
2. Kuwepo na njia bora ya kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa.
3. Kutoa fursa za kuhamasisha umma kuunga mkono miradi ya jamii ya maendeleo.
4. Kurahisisha utetezi, na kufanikisha mazungumzo kuhusu mabadiliko au maboresho katika utoaji huduma.
5. Kuwasaidia wananchi na jamii kuelewa michakato ya uwajibikaji katika ngazi tofauti za serikali.
6. Kuhimiza mashirika ya kijamii au umma (CSO) kushiriki katika mchakato wa 'ndani' wa uwajibikaji wa serikali.

---

[8]Kohli (2012)

# Mambo ya kuzingatia ili kutumia nyenzo za uwajibikaji wa kijamii kwa ufanisi na ipasavyo:

1. Kuelewa vyema muktadha wa kijamii na kisiasa.
2. Kutenga muda kuelewa mpangilio wa fedha za umma katika ngazi za kieneo, kikanda na kitaifa.
3. Kufuata utaratibu wa CCT katika kutambua na kuyapa kipaumbele mahitaji ya jamii ili kuhakikisha yameshughulikiwa.
4. Kusaidia jamii kubuni kikundi (kinachojulikana kama 'mabingwa wa uwajibikaji wa kijamii' katika mazingira fulani) ili kuongoza mchakato.
5. Kuhakikisha wanajamii wengine wanaelewa mchakato na wanatoa maoni mara kwa mara ili kuhakikisha wanachangia kikamilifu.
6. Kuhakikisha watoa huduma wanajizatiti kuanzia mwanzo.
7. Kuweka mpango maalum wa ufuatiliaji.

# Jinsi ya kutumia nyenzo hizi

1. Unapaswa kusisitiza umuhimu wa utetezi na kiini chake katika kila hatua ya mchakato wa CCT. Mwongozo wa utetezi wa masuala ya uhamasishaji wa kanisa na jamii (CCM) unaeleza jinsi ya kutekeleza hili, k.m. mambo ya kuzingatia wakati wa kuwateua viongozi wa utetezi wa CCT.
2. Michakato tofauti ya CCT hutumika katika mazingira tofauti, hivyo hakikisha unaelewa vyema utaratibu wa CCT unaotumika katika jamii ambapo utatumia nyenzo husika.
3. Unahitaji kutumia nyenzo hizi katika hatua sahihi ya mchakato; nyenzo nyingi katika mwongozo huu zinaweza kutumika katika hatua ambapo ubainishaji wa rasilimali tayari umefanywa. Kwa pamoja, kanisa na jamii zitakuwa zimepata nafasi ya kutathmini mahitaji yao, kubaini matatizo na fursa zilizopo katika jamii zao, kuweka kipaumbele matatizo wanayotaka kuzingatia, na zitakuwa zimeanza kukusanya rasilimali ili kushughulikia matatizo hayo. Kisha unaweza kutumia nyenzo sahihi ya uwajibikaji wa kijamii ili kuwasaidia kupata rasilimali za serikali za kushughulikia matatizo yao.
4. Mwongozo huu umeandaliwa katika muundo rahisi na unaoeleweka, hata hivyo, tunakuhimiza ufungue viungo vilivyo katika sehemu ya 'Mwongozo zaidi' kwa kila nyenzo ili upate maelezo zaidi kuhusu nyenzo na matumizi yake.


5. Kila nyenzo ina utaratibu wake ambao unaweza kubadilishwa ili kuendana na mahitaji ya kila muktadha au hali. Mwongozo huu utakusaidia kuwazia mambo ya kujumuisha unapotumia kila nyenzo.
6. Pana mfano wa utaratibu maalum mwishoni mwa kila nyenzo. Pia kuna kiungo cha kufungua toleo la utaratibu unaoweza kubadilishwa, na unaweza kupakua na kubadilisha ili kuendana na mazingira yako.

## Matumizi ya nyenzo za kidijitali za uwajibikaji wa kijamii

Nyenzo hizi zote zinaweza kuchapishwa au kutumika kidijitali ili kurahisisha upatikanaji wake kupitia mifumo tofauti ya teknolojia.

# Kutumia nyenzo katika mpango wa maendeleo ya serikali

Kutumia nyenzo katika mpango wa maendeleo ya serikali




Nyenzo za uwajibikaji wa kijamii zina ufanisi sana pale ambapo:

a) Zinaanzishwa na kuhusishwa na taratibu mbalimbali za utoaji huduma.[9]

b) Zinatumika katika hatua sahihi ya mpango wa maendeleo ya serikali.

Nyenzo nyingi za uwajibikaji wa kijamii huangazia hatua mbili za kwanza, kwani ndizo za kimsingi katika kufikia matokeo chanya. Kupanga bila kuyapa kipaumbele masuala muhimu, na pia utekelezaji duni wa mpango mzuri utapelekea matokeo yasiyofaa. Nyenzo ya CIVICUS kuhusu Kushirikisha Umma ni muhimu sana kwa usomaji wa kina.

[9] Kohli (2012)

Zifuatazo ni hatua za kawaida za mpango wa maendeleo ya serikali pamoja na baadhi ya nyenzo za uwajibikaji wa kijamii zinazotumika katika kila hatua, na zilizoangaziwa kwenye mwongozo huu.

| **Hatua za mpango wa maendeleo ya serikali** | **Hatua ya kwanza: Kufuatilia na kuchangia mipango ya kimkakati na kuandaa bajeti** | **Hatua ya pili: Kufuatilia utekelezaji wa miradi na mipango** | **Hatua ya tatu: Kufuatilia matokeo ya maendeleo** |
|---|---|---|---|
| **Swali muhimu linalojibiwa** | Je, mipango iliyobuniwa na fedha zilizotengwa zinatosha kufikia malengo yaliyowekwa? | Je, miradi/shughuli zinatekelezwa kulingana na ubora, mpango, na bajeti iliyowekwa? | Je, miradi na shughuli zinazotekelezwa zitatusaidia kufikia malengo/matarajio yetu? |
| **Nyenzo za uwajibikaji wa kijamii zinazopaswa kutumika, zinazopatikana katika mwongozo huu** | Mchakato wa mipango shirikishi | Ufuatiliaji wa bajeti | Ufuatiliaji wa bajeti |
| | Ufuatiliaji wa bajeti | Uandishi wa habari wa raia | Uandishi wa habari wa raia |
| | Uandishi wa habari wa raia | Kadi za tathmini ya jamii | Kadi za tathmini ya jamii |
| | Kadi za tathmini ya jamii | Uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma | Ukaguzi wa kijamii |
| | | Ukaguzi wa kijamii | |

Kwenye Kiambatisho utaona chati ya hatua muhimu za mpango wa kawaida wa maendeleo ya serikali

# Nyenzo ya mchakato wa mipango shirikishi



**Wanachama wa kamati andalizi ya kijiji cha Simayiwa 1 wakifanya mkutano na wanakijiji ili kuwaeleza kuhusu maendeleo ya baadaye.** Picha: Alex Baker/Tearfund

## Katika sehemu hii

Kuhusu nyenzo hii • Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha • Mwongozo zaidi • Mfano wa utaratibu • Utaratibu unaoweza kubadilishwa

# Kuhusu nyenzo hii

**Mipango shirikishini mchakato ambapo wanajamii huonyesha ushawishi na udhibiti wao katika mipango ya maendeleo inayowahusu. Wanafanya hivi kwa kushiriki pakubwa katika kuweka vipaumbele, kutenga rasilimali na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo.**[10]

Mipango shirikishi huwezesha wadau mbalimbali - wanajamii, mashirika ya kijamii (CBO), makanisa ya eneo, mashirika ya kiraia (CSO), maafisa wa serikali, n.k. - kushiriki katika kubaini na kuratibu miradi ya maendeleo inayotumia fedha za umma.[11]

Neno 'kushirikisha' linaweza kutumika kumaanisha michakato mbalimbali kama vile mashauriano au kushiriki taarifa. Tunahimiza ushirikiano katika kubuni mipango kwani inawezesha wanajamii kushiriki moja kwa moja katika usimamizi wa eneo lao. Inahusisha wanajamii katika kufanya maamuzi kuhusu kuweka vipaumbele kuhusu matatizo, kupata suluhu, kutekeleza hatua, kisha kufuatilia na kutathmini hatua hizo. Pia inajumuisha kutafuta na kudhibiti rasilimali.[12]

[10]World Bank (1996) uk.xi

[11] Oduor (2014)

[12] Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo (2002)

Ni endelevu kwani inaweza kupelekea kubuniwa kwa taratibu kama vile:

- uwakilishi wa wadau katika kufanya maamuzi
- kamati za kubuni mipango ya kieneo
- kuchangia kuunda bajeti
- mipango ya fedha ya kufadhili maendeleo yanayosimamiwa na jamii[13]

## Madhumuni ya nyenzo hii

Nyenzo hii inalenga kuunga mkono juhudi za makanisa na jamii kufanya yafuatayo:


- Kuhakikisha wananchi wanachangia katika mipango na miradi ya maendeleo ya serikali.
- Kuhakikisha jamii zinashiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi ya maendeleo yanayowahusu
- Kuhakikisha kwamba hatua za maendeleo zinaambatana na mahitaji na mapendeleo ya jamii husika.[14]

[13] CIVICUS: Kushirikisha Umma katika Mipango ya Maendeleo

[14] CIVICUS: Kushirikisha Umma katika Mipango ya Maendeleo

Ili unufaike zaidi kutokana na nyenzo hii, rejelea pia nyenzo zingine husika kama vile kadi za tathmini ya jamii (CSC) na ukaguzi wa kijamii. Hii ni kuhakikisha kuwa wanajamii wanapochangia katika kuweka mipango, wana ithibati – iliyokusanywa kwa kutumia kadi ya tathmini ya jamii (CSC) – na wanaweza kufuatilia kwa uwazi jinsi mipango iliyokubaliwa itakavyotekelezwa – kwa kutumia nyenzo ya ukaguzi wa kijamii.

Nyenzo hii inafaa zaidi kwenye jamii ambapo wananchi wangependa kushiriki katika kubuni mipango. Hata hivyo, inaweza kubadilishwa ili itumike kieneo na kitaifa.



## Ufaafu na upungufu wa nyenzo hii

**Ufaafu:**

- Inahimiza wananchi kutoa maoni. Wananchi waelewa vyema kuhusu mipango ya maendeleo kutokana na kushirikishwa katika michakato ya mipango ya serikali. Wana fursa kushiriki katika kutambua mahitaji ya maendeleo na katika kuteua sera na mpango ambayo inafaa kupewa kipaumbele na serikali za mitaa.
- Inawapa raia fursa ya kutathmini uwazi, utendakazi, na uwajibikaji wa serikali zao za mitaa. Wananchi kushirikishwa katika utekelezaji wa mipango na pia katika kufuatilia na kutathmini utendakazi wa serikali zao za mitaa.[15]
- Huwezesha wanajamii kuhusika katika mipango ya serikali za mitaa, na hivyo, hutoa fursa za ufikiaji wa rasilimali za jamii, kwa mfano rasilimali zilizobainishwa kwenye michakato ya uhamasishaji wa kanisa na jamii.[16]
- Husaidia katika kusawazisha uhusiano wa kimamlaka miongoni mwa viongozi tofauti, wadau, na rasilimali, hivyo kuwezesha wahusika kushirikiana kwa usawa na kwa ukaribu.

---

[15] Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo (2002)

[16] Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo (2002)

**Upungufu:**

- Huenda ikawazuia wanajamii kushiriki moja kwa moja katika utekelezaji, ufuatiliaji au kutathmini hatua zinazochukuliwa. Hata kukiwepo na mifumo madhubuti ya kisheria, huenda kusiwe na mazingira yanayohimiza mchango wa wananchi. Kwa mfano, huenda kusiwe na mwingiliano kati ya wananchi na serikali, au huenda wanajamii wasiwe wanahusika au wasiwe wanajua yanayoendelea, au huenda kusiwepo na usaidizi kutoka kwa wanasiasa.[17]
- Mchakato huo unaweza kutekwa na wasomi wa jamii au watu na mashirika mengine yenye uwezo ili kulinda maslahi yao wenyewe kwa kutumia hila kwenye mchakato.[18]
- Inachukua muda na rasilimali kuwashirikisha wadau mbalimbali wenye maslahi tofauti.
- Inaongeza matarajio. Kuwaomba wadau mbalimbali wachangie katika mchakato wa kubuni na kupanga sera kunaweza kuwapa matarajio kuwa mapendekezo yao yatatekelezwa; hili haliwezekani kila wakati, na mipaka hii inahitaji kuwekwa wazi kuanzia mwanzo.

[17] Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo (2002)

[18] CIVICUS: Nyenzo kuhusu Kushirikisha Umma

# Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha

## Je, nyenzo hii inatumika wapi kwenye mchakato wa CCT?

Michakato tofauti ya CCT hutumika katika mazingira mbalimbali. Hata hivyo, michakato yote ya CCT hutumia mbinu shirikishi, hivyo kuna fursa ya kuhusisha mipango shirikishi. Nyenzo hii ni mwafaka zaidi katika hatua ambapo kanisa pamoja na wanajamii wamefanya tathmini ya mahitaji yao, wamebaini matatizo, fursa na rasilimali katika jamii zao na wameanza kukusanya rasilimali ili kushughulikia matatizo hayo. Wanajamii tayari wana mtazamo mpya na wanatambua nafasi yao. Wako katika nafasi nzuri ya kubaini vipaumbele vinavyowekwa katika mipango ya serikali za mitaa, pamoja na kulinda maslahi ya jamii, na hata kushiriki katika juhudi za kuleta pamoja rasilimali zinazohitajika.

Endapo mojawapo ya rasilimali zinazohitajika ni ufadhili wa serikali za mitaa, kushiriki katika mipango ya serikali za mitaa kutawezesha maslahi ya wanajamii kupewa kipaumbele katika ugavi wa rasilimali na kwenye mipango ya serikali.

Zifutazo ni baadhi ya mbinu za CCT na mapendekezo ya mahali ambako nyenzo hii inaweza kutumika:

| Mbinu ya CCT | Mchakato wa uhamasishaji wa Kanisa na Jamii | Umoja/Parivartan/Unidos | Sangsangai |
|---|---|---|---|
| Wakati wa kutanguliza mipango shirikishi | **Hatua ya 4:** Uchambuzi wa taarifa<br><br>**Hatua ya 5:** Kufanya Uamuzi | **Hatua ya 3:** Kuweka malengo na kuchukua hatua (kupanga utekelezaji)<br><br>**Hatua ya 4:** Kuchukua hatua | **Awamu ya 3:** Jamii |

Kanisa na jamii wanaweza kukuza ujuzi wao katika mipango shirikishi kupitia mchakato ulioelezwa hapa chini.

## Kutumia nyenzo

Pana utaratibu mwishoni mwa mwongozo wa nyenzo hii.

**Ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilisha kulingana na hali iliyopo, tafadhali tembelea learn.tearfund.org/sa-tools**

Tafadhali kumbuka; mchakato wa CCT ni shirikishi, na majukumu mengi yaliyotajwa kwenye nyenzo ya mipango shirikishi yatakuwa yamefanywa na kanisa na jamii ikiwa wamekamilisha hatua ya 3 na 4 ya CCT.

Zoezi lililo hapa chini litafanywa haswa kwa masuala yanayohitaji kushughulikiwa kupitia usaidizi au kuhusika kwa serikali. Mkazo ni katika kubuni mpango unaobainisha jinsi ya kuhusisha mipango ya serikali ili kuhakikisha masuala ya jamii yanapewa kipaumbele na serikali. Zifuatayo ni hatua muhimu katika mchakato wa mipango shirikishi. Sampuli ya utaratibu ipo mwishoni mwa mwongozo huu.

1. **Mazungumzo kuhusu fursa na changamoto**
   Hii ni sawa na hatua ya 3 na 4 ya michakato mingi ya CCT ambapo tathmini hufanywa kubaini matatizo na rasilimali zilizopo ili wadau waweze kukubaliana kuhusu fursa zilizopo, na masuala yanayopaswa kupewa kipaumbele.

2. **Mikakati ya kijamii**
   Hii ni sawa na kupanga na kufanya maamuzi kwenye mchakato wa CCT. Katika hatua hii, wanajamii wanapaswa kubainisha wazi yafuatayo:
   - Hatua zitakazoshughulikia masuala yaliyobainishwa
   - Mahali ambako shughuli hizo zitafanyika
   - Kwa nini shughuli hizo zinapaswa kufanywa
   - Idadi inayokadiriwa ya watakaonufaika
   - Kinachopaswa kufanywa na wanajamii
   - Majukumu ya taasisi husika,
     mfano serikali

3. **Kubainisha fursa zilizopo**
   Tafuta fursa ambapo masuala yaliyobainishwa yanaweza kujumuishwa katika mipango na bajeti za serikali. Utahitaji:

   a. **Kufanya utafiti**
   Kujua sheria na sera zilizopo katika nchi yako kuhusiana na umma kushiriki katika mipango ya serikali.

   b. **Kujenga mahusiano**
   Ni muhimu sana kuwa na uhusiano mwema na maafisa wa idara husika za serikali au mamlaka ya mtaa, na pia viongozi wa jamii.

   c. **Kukubaliana kuhusu masuala yanayohitaji kujumuishwa katika mpango na bajeti ya serikali.**
   Hii inategemea vipaumbele na rasilimali zilizobainishwa katika utambuzi wa matatizo na uwekaji vipaumbele kwenye CCT Sio masuala yote yatakayojumuishwa katika mpango wa serikali kwani baadhi ya masuala hayo yatashughulikiwa na jamii kwa kutumia rasilimali zake zinazoambatana na kanuni za CCT.

d. **Kusanya taarifa unazohitaji**

Angalia miongozo ya mamlaka za eneo kuhusu kupanga na kuhusika kwa jamii ili kubaini ikiwa kuna mfumo wa kisheria unao unga mkono kushiriki kwa wananchi, na kuelewa mipango ya serikali iliyopo (ikiwa ni pamoja na tarehe muhimu za mipango). Baada ya kupata stakabadhi zote, zisome kwa makini. Usijali ikiwa una maswali kuhusu mambo ambayo huelewi - unaweza kuwauliza wahudumu ofisini au maafisa wa mamlaka waliotoa taarifa hiyo.

e. **Kubuni mkakati**

Kulingana na majibu kwenye nyenzo ya mipango shirikishi, makubaliano yatafikiwa kuhusu jinsi ya kushiriki katika mpango wa serikali ili kuhakikisha vipaumbele vya jamii vinashughulikiwa katika mipango na bajeti rasmi za serikali. Hii itajumuisha kukubaliana kuhusu majukumu.

## Ufaafu wa nyenzo hii
# Mfano

**Soma mtandaoni**
[Advocacy in Nepal: Training communities to work with local government]

**Nchini Nepal, serikali ya kitaifa ilibuni sheria inayowapa wananchi fursa ya kushiriki pakubwa katika miradi ya maendeleo, kupitia mchakato wa mipango shirikishi (PPP). Kwa mujibu wa sheria hiyo, serikali za mitaa zinapotenga fedha kwa ajili ya maendeleo, zinapaswa kuzingatia mapendekezo ya kamati za maendeleo vijijini (VDC). Hata hivyo, ukweli ni kuwa, wakati mwingi maamuzi yalifanywa na viongozi na wanasiasa wachache wenye ushawishi. Mara nyingi, maoni na mahitaji ya wanajamii hayakuzingatiwa.**

Ili kubadilisha mtindo huu, shirika la United Mission to Nepal (UMN), liliwahamasisha watu kutoka VDC kadhaa ili kuwasaidia wapate fursa zaidi za kushiriki katika maendeleo ya kijamii, na likatoa mafunzo kuhusu jinsi ya kupata fedha kupitia serikali za mitaa. Kwenye jamii, waliwahimiza pia waelekezi wa kijamii kutembelea kila nyumba na kuwaalika wajiunge na mkutano wa mwanzo. Waelekezi walikuwa na uhusiano wa muda mrefu na jamii zao na walikuwa na uelewa mpana wa muktadha wa hapo.

Hii ilimaanisha kuwa walikuwa na fursa ya kuhimiza hasa familia maskini na za tabaka la chini na makundi mengine yaliyotengwa kushiriki - kawaida watu hawa hawangejumuishwa.

Katika mikutano hiyo, wanajamii walijifunza kwamba fedha za maendeleo za VDC zilikuwa zao, na walikuwa na haki ya kutoa maoni kuhusu ugavi wa fedha hizo. UMN iliwafunza kuhusu mchakato wa serikali na masuala ya kipaumbele, pamoja na jinsi ya kuandaa pendekezo. Walihimiza wanajamii kutambua na kuyapa kipaumbele masuala, na kujadili suluhu. Pia waliwasaidia kuwazia na kupata rasilimali zingine, na kupata usaidizi wa kiufundi ilipohitajika. Wawakilishi wadi waliwasilisha mapendekezo ya wanajamii kwa VDC.

Kutokana na hatua hii ya wanajamii kushirikiana na serikali za mitaa kufanya maamuzi, fedha zilitolewa kufadhili miradi ya jamii. Miradi hii ilijumuisha mafunzo ya kushona kwa wanawake wasio na waume, nyenzo za vituo vya watoto wachanga, ukarabati wa mabomba ya unyunyizaji maji, ujenzi wa vyoo, jengo jipya la kanisa, na uzio wa kuzingira makabauri.

# Mwongozo zaidi

Unapopanga kutumia nyenzo hii kusaidia kanisa na jamii katika eneo fulani, unahitaji kukusanya habari ili uelewe mambo muhimu kuhusu mipango yao ya kitaifa na kieneo ili uwe na ujasiri kuhusu suala unaloangazia. Kisha utahitaji kufanya utafiti miongoni mwa wanajamii ili kuelewa kwa kina michakato ya kubuni mipango katika eneo lao.

Maswali muhimu ya kuangaziwa:

- Je, kuna sheria inayounga mkono mipango shirikishi?
- Je, mwaka wa fedha unaanza na kukamilika lini?
- Mipango ya kila mwaka hubuniwa vipi kieneo na kitaifa?
- Je, chaguo zipi zinapatikana za kuchangia katika mipango ya kieneo au kitaifa?
- Je, ni nani anayeongoza mchakato wa kubuni mipango?
- Je, ni tarehe gani muhimu, k.m. tarehe ya mwanzo na ya mwisho ya vipindi vya mashauriano?

## Viungo vya hati na nyenzo zaidi zinazohusiana na mipango shirikishi

a. Utetezi nchini Nepal:  Kushirikisha umma katika kubuni mipango ya serikali

b. 2.1.4 Mbinu na nyenzo zilizotumika za mipango shirikishi

c. Participatory Development Planning

## Faharasa

**Bajeti:** Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi fulani.

**Maendeleo yanayosimamiwa na jamii:** Mchakato ambapo wanajamii hushirikiana ili kuchukua hatua za pamoja na kupata suluhu kwa matatizo yanayowakabili.

**Mwaka wa fedha:** Kipindi cha miezi kumi na miwili (sio lazima iwe tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba) ambapo serikali au biashara hupanga bajeti.

**Serikali:** Ofisi, idara, na makundi ya watu wanaoendesha nchi, jimbo, jiji, au asasi nyingine ya kisiasa.

**Mpango:** Maamuzi kuhusu jinsi ya kutekeleza mambo fulani siku za mbeleni.

**Sera ya umma:** Sera ya umma ni hatua inayochukuliwa na kuidhinishwa na serikali ili kufikia malengo fulani. Hii inaweza kufanyika kwa njia nyingi. Kwa mfano, inaweza kuwa sheria, mkakati au mpango. Hata hotuba ya rais au waziri inaweza kuelezea mpango wa serikali.

# Sampuli ya mwongozo

## Mwongozo wa mchakato wa mipango shirikishi

| **Nchi** | **Tarehe** |
|---|---|
| | |
| **Jina la utawala la eneo husika** | |
| | |
| **Jina la jamii/kijiji** | |
| | |
| **Mradi/huduma za umma za kujumuishwa katika mpango wa serikali:** | |
| **1.** | |
| **2.** | |
| **3.** | |

<table>
<tr><th>Masuala kuu</th><th>Majibu</th></tr>
<tr><td>1. Je, ukadiriaji wa matatizo na fursa umefanyika?<br><br>Orodha hii ya matatizo na fursa inapaswa kushirikiwa ikiwa jamii imefanya yafuatayo kwenye mchakato wa CCT: kukusanya na kuchambua taarifa; kuweka malengo; kupanga au kuchukua hatua.</td><td>☐ Ndiyo<br><br>☐ La</td></tr>
<tr><td colspan="2">Maoni na maelezo</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td>2. Je, fursa zilizopo zimebainishwa ili wanajamii waweze kushiriki katika mipango ya serikali?</td><td>☐ Ndiyo<br><br>☐ La</td></tr>
<tr><td colspan="2">Maoni na maelezo</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
</table>

| Masuala kuu | Majibu |
|---|---|
| 2.1. **Je, pana mfumo wa kisheria unaowezesha wananchi kushiriki katika mchakato wa kupanga?** | ☐ **Ndiyo**<br>☐ **Ndiyo – Kushiriki taarifa**<br>☐ **Ndiyo – Kushauriana na wanajamii**<br>☐ **Ndiyo – Kubuni mipango kwa kushirikisha umma**<br>☐ **Ndiyo – Nyingine**<br>☐ **La**<br>(Ikiwa LA, nenda swali la 2.2.) |
| **Maoni na maelezo** | |
| | |

| **Masuala kuu** |
| --- |
| 2.1.1. **Je, mipango ipi ya serikali inapatikana katika kiwango chako cha utawala?**<br><br>Ni ipi bora kwako kushiriki, ili matatizo yako kuu yajumuishwe katika mipango ya serikali? |
| **Maoni na maelezo** |
| |
| 2.1.2. **Je, tarehe muhimu za mipango ya serikali ni zipi?**<br><br>• Mchakato wa kubuni mipango huanza mwezi gani?<br>• Mashauriano huanza na kuisha lini?<br>• Mpango na bajeti rasmi ya serikali itakuwa tayari lini? |
| **Maoni na maelezo** |
| |

<table>
<tr><th>Masuala kuu</th><th>Majibu</th></tr>
<tr><td>2.1.3. Je, serikali hupokea vipi mawasilisho kutoka kwa wanajamii?<br>• Je, taarifa zako (kutokana na mchakato wa CCT) zinapatikana katika muundo unaohitajika?<br>• Je, ni nani amechaguliwa kutoa mawasilisho kwa niaba ya wanajamii?</td><td>☐ Mawasilisho yaliyoandikwa<br>☐ Mikutano ya mashauriano ya kijamii<br>☐ Warsha za kubuni mipango</td></tr>
<tr><td colspan="2">Maoni na maelezo</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
<tr><td>2.1.4. Je, kuna fursa nyingine maalum za jamii kushiriki?<br>Kwa mfano, asilimia fulani ya fedha za maendeleo kutengwa kwa ajili ya miradi iliyochaguliwa na wanajamii?</td><td>☐ Ndiyo<br>☐ La</td></tr>
<tr><td colspan="2">Maoni na maelezo</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td></tr>
</table>

| Masuala kuu | Majibu |
| --- | --- |
| 2.2. **Ikiwa hakuna mfumo wa kisheria unaowezesha wananchi kushiriki katika kubuni mipango:**<br><br>**2.2.1. Je, kuna fursa za kuanzisha au kudumisha uhusiano na wakuu waliobainishwa kwenye tathmini ya kitaasisi kupitia CCT, na kuwaeleza vipaumbele vya jamii mchakato unapoanza?**<br><br>• Je, taarifa zako (kutokana na mchakato wa CCT) zinapatikana katika muundo unaohitajika?<br><br>• Je, ni nani amechaguliwa kutoa mawasilisho kwa niaba ya wanajamii? | ☐ **Ndiyo**<br><br>☐ **La** |

| Maoni na maelezo |
| --- |
| |

| Masuala kuu | Majibu |
| --- | --- |
| **2.2.2.** Je, kuna fursa za kuchangia katika kubuni mipango ili masuala ya jamii yaendelee kuangaziwa katika mipango? | ☐ Ndiyo<br>☐ La |
| **Maoni na maelezo** | |
| | |
| **2.2.3.** Je, kuna fursa za kutetea kuanzishwa kwa mfumo wa kisheria unaohitaji wananchi kushiriki katika mipango ya serikali? | ☐ Ndiyo<br>☐ La |
| **Maoni na maelezo** | |
| | |

## Mwongozo kuhusu hatua za haraka ikiwa serikali tayari imeidhinisha mpango na bajeti yake

3. **Kupitia mipango na bajeti iliyoidhinishwa ili kubaini ikiwa vipaumbele vya jamii vimeangaziwa**

- Kwa usaidizi wa viongozi wa jamii, wasilisha ombi kwa maafisa wasimamizi ili waeleze wanajamii kuhusu mipango na bajeti ambayo tayari imeidhinishwa. Hii ni taarifa muhimu katika kufuatilia utekelezaji wa miradi kwa kutumia nyenzo zingine za uwajibikaji wa kijamii, k.m. ufuatiliaji wa matumizi ya umma, kadi ya tathmini ya jamii, au ukaguzi wa kijamii.
- Iwapo vipaumbele vya jamii havijaangaziwa, bainisha sababu kisha wazia jinsi ya kufadhili vipaumbele vya jamii kwa kutumia vyanzo vingine, au subiri hadi awamu ijayo ya kubuni mipango.
- Wanajamii wanapaswa kuafikiana kuhusu mchango wao kwa pamoja ili kuhakikisha mafanikio ya mipango hiyo.
- Kuwauliza wakuu kuhusu changamoto wanazotarajia, kisha mkubaliane kuhusu jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo.
- Kukubaliana kuhusu mara ngapi mikutano inapaswa kufanyika kati ya wanajamii na maafisa wasimamizi.

| **Maoni na maelezo** |
| --- |
| |

**Tembelea learn.tearfund.org/sa-tools ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilisha kulingana na hali iliyopo.**

# Nyenzo ya ufuatiliaji wa bajeti



**Kikundi cha kusaidiana (Grupo de Ahorro) huko Las Flores kinachoungwa mkono na Tearfund kupitia mshirika wetu wa ndani - AGAPE.** Picha: Linda Esperanza Aragon/Tearfund

## Katika sehemu hii

Kuhusu nyenzo hii • Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha • Mwongozo zaidi •Mfano wa utaratibu • Utaratibu unaoweza kubadilishwa

# Kuhusu nyenzo hii

**Nyenzo hii inatumika na wananchi, wanajamii, na wadau wengine husika kufuatilia matumizi ya serikali kupitia uchambuzi na ukaguzi wa bajeti unaofanywa mara kwa mara.**

Ufuatiliaji wa bajeti unahusisha kufanya yafuatayo:

1. Ukaguzi: Kuangalia mgao wa fedha na kubaini ikiwa fedha hizo zimetengewa sekta zinazofaa.
2. Uchambuzi wa bajeti: Kuangalia kiasi kilichotengwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha na kufuatilia kiasi kilichotolewa, na kiasi kilichotumika. Kujibu swali: 'Je, hili linatuelekeza kufikia maendeleo yaliyokusudiwa?'

## Madhumuni ya nyenzo hii

Kufuatilia ugavi wa fedha ili kuhakikisha zimetengwa ipasavyo, zinatolewa kwa wakati na zinatumika kama ilivyopangwa (kulingana na bajeti).

Nyenzo hii inaweza kutumika katika ngazi zote za serikali palipo na uundaji bajeti au matumizi ya fedha.

## Ufaafu na upungufu wa nyenzo hii

### Ufaafu

- Inasaidia katika utekelezaji kamilifu wa bajeti zilizowekwa: bajeti inaashiria ‘machaguo ya serikali katika kufikia ajenda yake ya kijamii na kiuchumi. Hivyo, ufanisi katika utekelezaji wa bajeti unadhihirisha jinsi malengo yanavyotimizwa kupitia sera zilizopo.’[19]
- Utoaji huduma unaweza kuboreshwa ikiwa fedha za bajeti zinatumika ipasavyo badala ya kucheleweshwa au kuelekezwa kwingine.
- Inaweza kutumika kuzuia na kufichua ufisadi, uhalifu na matumizi mabaya ya rasilimali, kwa kuwa wananchi wanaweza kugundua ikiwa fedha zinatumika vibaya.

[19] Kohli (2012) akinukuu Aiyar na Behar (2005)

**Upungufu**

- Wanaoathirika zaidi kutokana na maamuzi huenda wasiwe na fursa ya kushiriki katika mchakato huo: ugavi wa rasilimali unaweza kuegemea upande fulani kutokana na misimamo au mahitaji ya kibinafsi. Huenda pia kukawa na hila za kisiasa. Wanaoathirika zaidi huenda wasiwe na ubabe wa kisiasa au kiuchumi, na hivyo kuwatenga katika kushiriki kwenye mchakato wa uundaji wa bajeti.[20]
- Hakuna uhakika ikiwa rasilimali zilizojumuishwa kwenye bajeti zitapatikana kufadhili mipango mbalimbali.
- Ni vigumu kutumia nyenzo hii katika mfumo wa serikali kuu.[21]

[20]Kohli (2012)

[21]Ni rahisi zaidi kuitumia katika utawala wa ugatuzi ambapo mamlaka ya kisiasa, kifedha na kiutawala yamehamishwa kutoka serikali kuu hadi serikali za mitaa (wilaya/jiji), ili serikali iweze kurahisisha na kuhakikisha huduma bora kwa umma. Cifor

# Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha

## Je, nyenzo hii inaweza kutumika katika hatua gani ya CCT?

Michakato tofauti ya CCT hutumika katika mazingira mbalimbali. Nyenzo hii ni mwafaka zaidi baada ya ubainishaji wa rasilimali kufanyika. Kanisa pamoja na wanajamii wamefanya tathmini ya mahitaji yao, wamebaini matatizo na fursa katika jamii zao,  na wameyapa kipaumbele matatizo wanayotaka kuangazia, na wameanza kukusanya rasilimali ili kushughulikia matatizo hayo. Ni katika hatua hii ambapo nyenzo hii inaweza kutumika kwani wanajamii wanaelewa vyema matatizo yanayohitaji yashughulikiwe na kupitia bajeti ya serikali.

Zifutazo ni baadhi ya mbinu za CCT na mapendekezo ya mahali ambako nyenzo hii inaweza kutumika:

| Utaratibu wa CCT | Mchakato wa Uhamasishaji wa Kanisa na Jamii | Umoja/Parivartan/Unidos | Sangsangai |
|---|---|---|---|
| Wakati wa kutanguliza ufuatiliaji wa bajeti | **Hatua ya 4:**<br>Uchambuzi wa taarifa | **Hatua ya 3:**<br>Kuweka malengo na kuchukua hatua (kupanga utekelezaji)<br><br>**Hatua ya 4:**<br>Kutekeleza | **Awamu ya 3:**<br>Jamii |

Kanisa na wanajamii wanaweza kufunzwa kuhusu kufuatilia bajeti zinazowavutia kwa kutumia utaratibu ulioonyeshwa mwishoni mwa nyenzo hii.

## Kutumia nyenzo

**Kuandaa bajeti:** Shughuli hii ya kikundi, itakayoongozwa na waelekezi, husaidia kuonyesha mchakato wa bajeti.



Somo kuu ni kwamba 'familia' zinawakilisha serikali tofauti. Wapo walio na rasilimali nyingi kuliko wengine lakini wote hupanga, na bajeti wanazotengeneza zinadhihirisha vipaumbele vyao.

Kila familia hupanga na kuandaa bajeti, baadhi yao hupanga kwa imani kwani hawajui kiasi cha pesa watakachopata. Kama mwelekezi:

- Buni majina ya familia na uwape kazi zinazojulikana katika jamii/nchi yako.
- Hakikisha pana familia yenye kipato cha juu, familia ya tabaka la kati na familia inayopata kipato cha kila siku (hakuna ajira rasmi).
- Kwa kutumia sarafu ya nchi yako, onyesha kiasi ambacho kila familia inapata kila mwezi na idadi ya watoto katika kila familia.
- Wape kila familia jina kisha panga washiriki katika vikundi.
- Kila kikundi kinapaswa kuandaa bajeti ya mwezi.

- Kisha kila familia iwasilishe bajeti yake kwa kikundi, ikielezea sababu za kufanya maamuzi yao.
- Ongoza mazungumzo ili kuwasaidia washiriki kuwazia yaliyo kwenye bajeti.
- Jadili tofauti za vipaumbele kati ya familia, ikiwa zipo.
- Jadili kitakachotokea endapo pesa hazitatumika kulingana na bajeti ya familia. Kwa mfano, chukulia Bw. Koffi anatumia 700 kwa pombe. Je, hilo litaathiri vipi familia mwezi huo? Au familia ya Mwale ichangie 5,000 kwa harusi ya familia?



Jina la familia na kazi zao

| Idadi ya watoto | Jumla ya mapato | Mali | Kwa mfano, chukulia Bw. Koffi anatumia 700 kwa pombe. |
|---|---|---|---|
| **1. Familia ya Mwale Daktari na mkurugenzi wa kampuni** | 4 | 80,000 | Magari 3<br>Wanamiliki nyumba yao |
| **2. Familia ya Smith Mwalimu na mhudumu wa benki** | 3 | 20,000 | Gari 1<br>Wanaishi nyumba ya kukodi |
| **3. Familia ya Koffi Mfanyakazi wa nyumbani na kijakazi** | 4 | 700 na kiasi kingine chochote kutegemea mapato ya siku hiyo. | Baiskeli 1<br>Wanaishi nyumba ya kukodi |
| **4. Bw Keita (Hana familia) Mekanika** | 0 | 5000 | Amekodi chumba kimoja |

## Mchakato wa ufuatiliaji wa bajeti[22]

Zifuatazo ni hatua muhimu katika ufuatiliaji wa bajeti kwa kutumia utaratibu wa ufuatiliaji wa bajeti ulio hapa chini.

1. **Kuunda timu ya ufuatiliaji wa bajeti:** Ikiwezekana, wanachama wanapaswa kuteuliwa na wanajamii. Idadi ya wanachama hutofautiana, lakini kawaida huwa kati ya tisa na 14. Inapaswa kujumuisha wanawake na wanaume, na watu wa umri, kabila na hadhi tofauti kwenye jamii.
2. **Kufanya utafiti:** Kujua sheria na sera zinazotekelezwa nchini kwenu kuhusiana na uwazi wa bajeti. Kwa mfano, huenda kuna sheria zinazowaruhusu watu kushirikishwa kwa taarifa kuhusu bajeti.
3. **Kujenga mahusiano:** Ni muhimu sana kujenga uhusiano na watu katika idara husika ya serikali au mamlaka ya mitaa, na viongozi wa jamii.

[22]Kufuatilia matumizi ya fedha ya serikali, inarejelea Nyenzo ya REVEAL ya Tearfund.

4. **Kukubaliana kuhusu suala linalofaa kufuatiliwa kulingana** na masuala muhimu yaliyobainishwa kwenye CCT kuhusiana na kubaini matatizo na kuweka vipaumbele.

    a. **Kusanya taarifa za bajeti unazohitaji:** Kupata taarifa unazohitaji kuhusu mipango na bajeti ya mamlaka ya kieneo. Baada ya kupata stakabadhi zote, zisome kwa makini. Usijali ikiwa una maswali kuhusu mambo ambayo huelewi – unaweza kuwauliza wahudumu ofisini au maafisa wa mamlaka waliokupa bajeti hiyo.

    b. **Kujua kinachoendelea:** Je, bajeti inatumika inavyopasavyo?

    c. **Kagua maelezo yote:** Kila kitu kiko sawa?

    d. **Toa maoni kwa jamii yako** na ubainishe jinsi ya kufuatilia. Kusanya maelezo yote kisha ufanye mkutano wa wanajamii ili kuhakikisha watu wote wana fursa ya kusikia ripoti yako na kushiriki katika ufuatiliaji wowote.

## Ufaafu wa nyenzo hii

# Mfano

**Soma mtandaoni**

Utetezi nchini Bolivia

Kupitia mafunzo kuhusu ustawi wa kanisa na jamii (CCT), kanisa fulani nchini Bolivia liliunga mkono wanajamii katika kushawishi serikali ya mtaa kuboresha usambazaji wa maji katika eneo lao. Kupitia usaidizi kutoka kwa kanisa, wanajamii walishiriki katika kuandaa bajeti na kufuatilia matumizi ya fedha zilizotengwa hadi miundombinu ya usambazaji wa maji ilipojengwa. Hii ilisaidia kuboresha udhibiti wa taka na usambazaji maji kwa familia mbalimbali.

## Jinsi ufuatiliaji wa bajeti ulivyochangia katika ustawi wa jamii

Huko Tipa Tipa, kwenye jamii ya mashinani nchini Bolivia, maji ilikuwa nadra na hili liliathiri pakubwa maisha ya watu manyumbani. Licha ya mpango madhubuti wa wanajamii kuchimba mitaro ya kumwagilia mimea yao maji, manyumbani walikosa maji kwa muda mrefu.

Baada ya kupokea mafunzo ya CCT, kanisa la Tipa Tipa lilijitahidi kuisaidia jamii yao kupata maji. Pia walielewa kuwa masuala haya ya maji na usafi wa mazingira yalikuwa jukumu la serikali. Kanisa liliona fursa ya kuhakikisha wakaaji wa Tipa Tipa

wanapata maji baada ya serikali ya Bolivia kupitisha sheria mpya inayoruhusu wananchi kushiriki katika mgao wa bajeti. Kanisa la Tipa Tipa lilishawishi serikali ya mtaa kusambaza maji kwa wanajamii kwa kutenga bajeti ya kujenga tangi jipya la maji pamoja na mabomba ya maji kwa kila nyumba.

Baada ya mikutano mingi, serikali ya mtaa ilikubaliana na wanajamii kwamba serikali itatoa bajeti kufadhili mradi huu nao wanajamii watatenga muda wao na kujenga mabomba haya mapya ya maji. Isitoshe, kanisa la Tipa Tipa lilichangia katika mpango wa utendakazi wa kila mwaka wa manispaa na ujenzi wa bomba la maji taka huko Tipa Tipa. Familia ziliweza kuunganisha vyoo na bafu zao kwenye bomba hilo, na wanajamii waliweza kujenga bafu katika sehemu ambapo awali walikuwa na vyoo pekee.

# Mwongozo zaidi

Unapopanga kutumia nyenzo hii kusaidia kanisa na jamii fulani, unahitaji kukusanya habari ili uelewe mambo muhimu kuhusu uundaji wa bajeti ya kieneo na kitaifa, na utekelezaji wake nchini ili uwe na ujasiri kuhusu suala unaloangazia. Kisha utahitaji kufanya utafiti na jamii ili kuelewa kwa kina kuhusu michakato ya upangaji bajeti katika eneo lao.[23]

Maswali muhimu ya kuangaziwa:

1. Je, nchini bajeti hupitishwa lini kieneo na kitaifa?
2. Ni aina gani ya serikali iliyopo? Utawala ni wa serikali kuu au ya ugatuzi?
3. Ni rasilimali gani husambazwa nyanjani?
4. Taarifa za bajeti zinapatikana vipi?
5. Tarehe muhimu za mgao wa bajeti, utoaji fedha na utoaji wa taarifa ni zipi?

---

[23]Ingawa nyenzo hii inaweza kutumika kivyake, matokeo yake yanaweza kuimarishwa inapotumika baada ya Nyenzo ya mipango shirikishi

## Viungo vya hati na nyenzo zaidi zinazohusiana na ufuatiliaji wa bajeti

a. Kufuatilia matumizi ya fedha ya serikali (ufuatiliaji wa bajeti)

b. ufuatiliaji wa bajeti  ufuatiliaji wa bajetiUfuatiliaji wa bajeti kwa wanaoanza: Mwongozo wa utangulizi

c. Mwongozo kuhusu Uwajibikaji wa Kijamii: Mikakati na Nyenzo.Ukurasa wa 52 hadi 80 zinafafanua kwa kina kuhusu Ufuatiliaji wa bajeti.

d. Utawala wa Mitaa wa Haki na Demokrasia: Bajeti

e. Nyenzo za Warsha ya Mafunzo kwa Waelekezi na Washiriki kuhusu Bajeti za Kaunti nchini Kenya

## Faharasa

**Bajeti:** Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi fulani.

**Serikali kuu:** Serikali ambayo mamlaka ya utendaji na ya kutunga sheria yamejikita katika ngazi ya juu badala ya kusambazwa katika serikali mbalimbali za ngazi ya chini.

**Maendeleo yanayosimamiwa na jamii:** Mchakato ambapo wanajamii hushirikiana ili kuchukua hatua za pamoja na kupata suluhu kwa matatizo yanayowakabili.

**Ugatuzi:** Kukabidhi udhibiti wa shughuli au shirika kwa ofisi au mamlaka kadhaa za mitaa badala ya moja.

**Mwaka wa fedha:** Kipindi cha miezi kumi na miwili (sio lazima iwe tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba) ambapo serikali au biashara hupanga bajeti.

**Serikali:** Ofisi, idara, na makundi ya watu wanaoendesha nchi, jimbo, jiji, au asasi nyingine ya kisiasa.

**Mpango:** Maamuzi kuhusu jinsi ya kutekeleza mambo fulani siku za mbeleni.

**Sera ya umma:** Sera ya umma ni hatua inayochukuliwa na kuidhinishwa na serikali ili kufikia malengo fulani. Hii inaweza kufanyika kwa njia nyingi. Kwa mfano, inaweza kuwa sheria, mkakati au mpango. Hata hotuba ya rais au waziri inaweza kuelezea mpango wa serikali.

# Sampuli ya mwongozo

## Utaratibu wa ufuatiliaji wa bajeti[24]

| **Nchi** |
|---|
| |
| **Jina la jamii/kijiji** |
| |
| **Jina la utawala la eneo husika** |
| |
| **Mradi/huduma ya umma iliyoteuliwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa bajeti** |
| |
| **Kipindi cha ufuatiliaji wa bajeti** |
| |

[24]Inarejelea *Nyenzo ya Ushirika wa Kiinjili ya Kufuatilia Bajeti* ya Fedha za Maendeleo ya Eneo-bunge (CDF) nchini Zambia (2015).

## Kufuatilia mchakato na utekelezaji wa mradi fulani[25]

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina la mradi** | | | |
| **Kufuatilia mchakato** | | | |
| | **Ndiyo** (Tafadhali fafanua) | **La** (Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika** (Tafadhali fafanua) |
| **1. Je, wanajamii wanajua kuhusu mradi huu?** | | | |

[25]Tumia mbinu zile-zile zilizotumika wakati wa CCT kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa kwa wadau husika.

| | **Ndiyo** (Tafadhali fafanua) | **La** (Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika** (Tafadhali fafanua) |
|---|---|---|---|
| **2. Je, wanajamii wanajua kuhusu kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya mradi huu?** | | | |
| **3. Je, wanajamii walihusika katika kuteua mradi? K.m. Je, wanajamii walichangia katika kubuni mipango ya mradi huo?** | | | |
| **4. Je, wanajamii walihusika katika utekelezaji wa mradi? K.m. Je, walichangia kitu chochote/walitenga muda wao?** | | | |

| | **Ndiyo** (Tafadhali fafanua) | **La** (Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika** (Tafadhali fafanua) |
|---|---|---|---|
| **5. Je, wanajamii waliteua wauzaji bidhaa na watoa-huduma kwenye mradi huo?** | | | |
| **6. Je, mamlaka ya eneo ilitangaza hadharani fursa za usambazaji bidhaa na utoaji huduma?** | | | |

| Kufuatilia utekelezaji wa mradi | | | |
|---|---|---|---|
| **7.** Je, fedha kiasi gani zilitengwa kwa ajili ya mradi huu? (Pata taarifa kutoka kwa mamlaka ya eneo) | | | |
| | **Ndiyo** (Tafadhali fafanua) | **La** (Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika** (Tafadhali fafanua) |
| **8.** Je, vifaa vilivyonunuliwa na mamlaka ya eneo ni sawa na jinsi ilivyo kwenye pendekezo? | | | |
| **9.** Je, muuzaji alikusudiwa kupokea kiasi gani (kulingana na mamlaka ya eneo)? | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **10. Je, muuzaji anadai amepokea kiasi gani?** | | | |
| | **Ndiyo**<br>(Tafadhali fafanua) | **La**<br>(Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika**<br>(Tafadhali fafanua) |
| **11. Je, mradi umekamilika? (Tembelea mradi)** | | | |
| **12. Je, wanajamii wanahisi mradi utawafaa? (Swali la wanajamii)** | | | |
| **13. Je, wanajamii wanahisi mradi ni wa hali ya juu? (Swali la wanajamii)** | | | |

| **Kuuliza/kupata majibu kutoka kwa mamlaka ya eneo<br>(Haya ni maswali ya mwongozo, badilisha kulingana na muktadha)** | | | |
|---|---|---|---|
| | **Ndiyo**<br>(Tafadhali fafanua) | **La**<br>(Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika**<br>(Tafadhali fafanua) |
| **14. Je, wanajamii walihusika katika kuteua mradi?** **K.m. Je, wanajamii walichangia katika mikutano ya kubuni mipango?** | | | |
| **15. Je, wanajamii walihusika katika utekelezaji wa mradi?** **K.m. Je, walichangia kitu chochote/walitenga muda wao?** | | | |

| | **Ndiyo** (Tafadhali fafanua) | **La** (Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika** (Tafadhali fafanua) |
|---|---|---|---|
| **16. Wauzaji bidhaa na watoa huduma walichaguliwa vipi? Je, waliteuliwa na wanajamii? Je, ilikuwa kupitia zabuni ya umma?** | | | |
| **17. Je, fedha kiasi gani zilitengwa kwa ajili ya mradi huu?** | | | |
| **18. Je, vifaa vilivyonunuliwa na mamlaka ya eneo ni sawa na jinsi ilivyo kwenye pendekezo? Ikiwa si hivyo, sababu ni nini?** | | | |


| | **Ndiyo** (Tafadhali fafanua) | **La** (Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika** (Tafadhali fafanua) |
|---|---|---|---|
| **19. Muuzaji anatakiwa kupokea kiasi gani?** | | | |
| **20. Je, kuna ripoti ya tathmini ya mradi?** | | | |
| **21. Je, mradi umekumbwa na changamoto zozote?** | | | |

| Kukusanya majibu unapozuru mradi (Ukaguzi wa mradi) | | | |
|---|---|---|---|
| | **Ndiyo** (Tafadhali fafanua) | **La** (Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika** (Tafadhali fafanua) |
| **22. Je, vifaa vinavyonunuliwa na mamlaka ya eneo ni sawa na ilivyo katika mpango wa mradi/bajeti/orodha ya vipimo?** | | | |
| **23. Je, ubora wa vifaa unatosha?** | | | |

| | **Ndiyo** (Tafadhali fafanua) | **La** (Tafadhali fafanua) | **Sina uhakika** (Tafadhali fafanua) |
|---|---|---|---|
| **24. Je, muuzaji anadai amepokea kiasi gani?** | | | |
| **25. Je, mradi umekamilika?** | | | |
| **26. Je, mradi umekumbwa na changamoto zozote?** | | | |

**Tembelea learn.tearfund.org/sa-tools ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilisha kulingana na hali iliyopo.**

# Nyenzo ya uandishi wa habari wa raia



Mwanajamii anarekodi video ya wanajamii waliojitolea wakizuru shule nchini Bangladesh. Picha: Aaron Koch/Tearfund

## Katika sehemu hii

Kuhusu nyenzo hii • Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha • Mwongozo zaidi •Mfano wa utaratibu • Utaratibu unaoweza kubadilishwa

# Kuhusu nyenzo hii

**Uandishi wa habari wa raia hutekelezwa na raia wa kawaida wasio na uzoefu katika uandishi wa habari, na inahusu kuandaa simulizi zinazolenga hadhira fulani kwa kutumia simu ya mkononi yenye kamera na kinasa sauti, kisha kuzishiriki na wanajamii wenza au kuzisambaza kote kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari.**

Simulizi zinazoundwa kupitia uandishi wa habari wa raia mara nyingi huangazia jamii na masuala yanayopuuzwa na vyombo vya habari. Uandishi wa habari wa raia:

- unaweza kufanywa na mtu yeyote
- Huangazia masuala yasiyoangaziwa na vyombo vya habari
- huwapa wananchi fursa ya kuchangia kwenye jamii
- huwapa wananchi fursa ya kukusanya, kuchambua, kuripoti, na kusambaza taarifa kwa hadhira

## Madhumuni ya nyenzo hii

Kuwezesha waliotengwa wasikike kuhusiana na masuala yasiyoangaziwa na vyombo vya habari[26] na kuimarisha mshikamano wa kijamii na kitamaduni miongoni mwa wanajamii.

Nyenzo hii inaweza kutumika katika ngazi zote za utawala ambapo kuna upande wa mahitaji (raia) na upande wa wanaoshughulikia mahitaji (serikali).



[26]Kuwasiliana na vijiji vilivyo mbali, vilivyotawanyika au maeneo ambako idadi kubwa ya watu ni maskini. Huenda hadhira lengwa haijafikiwa na elimu au vyombo vya habari. Kumar (2021)

## Ufaafu na upungufu wa nyenzo hii

### Ufaafu

- **Hulinda uhuru wa kujieleza na maslahi ya raia:** Simulizi zinazotungwa na wanahabari wa raia huangazia kinachoendelea mashinani. Uandishi wa habari wa raiani 'njia mbadala ya kuripoti habari nyeti za kisiasa na kutoa nafasi ya umma kujadiliana mtandaoni, hivyo, kuwezesha sauti za wananchi wa kawaida kusikika.'[27]
- **Huunganisha wananchi na watunga sera:** Waandishi wa habari wa raia wakipata mafunzo ya kutosha, wanaweza kuwa vyanzo vya kuaminika vya habari kwa jamii zao, na kuziba pengo hili.
- **Kujua ukweli:** Nyenzo hii inaweza kufaa sana katika kutambua na kuthibitisha taarifa kunapotokea machafuko.
- Vifaa vinavyotumiwa na waandishi habari wa raia si ghali, ni faafu, na rahisi kutumia.

[27] Xin (2010)

**Upungufu**

- **Wanaoathirika zaidi huenda wakakosa kusikizwa:** Wakati mwingine, waandishi wa habari wa raia hawana wafuasi wengi.
- Wanasiasa, waandishi wa habari, raia, na wasomi huenda wakakubali tu kile wanachoamini au kuhisi ni kweli kulingana na hisia zao au maslahi yao. Hiki ni kizingiti cha kimaadili katika uandishi wa habari kwenye karne ambapo watu wanajali zaidi kuhusu hisia.[28]
- Huenda ikapuuza suala la kujidhibiti au kuzingatia viwango vya maadili: Hii inaweza pia kusababisha kuenea kwa habari za kupotosha.
- **Inaweza kusababisha vitisho kwa mtu binafsi:** Huenda mwandishi wa habari wa raia akakumbana na hatari za kimwili (kushambuliwa, kutekwa nyara, kufungwa jela, au kuuawa) au hatari za kidijitali (kunyanyaswa mtandaoni, kufuatiliwa, kukosa mawasiliano salama).[29]

---

[28] White A. (2017) Ethics in the News: EJN Report on Challenges for Journalism in the Post-truth Era.

[29]Vitisho vya kidijitali vinaweza kutoka kwa wananchi au serikali: Usalama wa Kidijitali

# Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha

## Je, nyenzo hii inatumika katika hatua gani ya mchakato wa CCT?

Michakato tofauti ya CCT hutumika katika mazingira mbalimbali. Nyenzo hii ni mwafaka zaidi baada ya kanisa na wanajamii kutathmini mahitaji yao, kubainisha matatizo yanayowakabili na fursa zilizopo katika jamii zao, na wameanza kukusanya rasilimali ili kushughulikia matatizo hayo. Iwapo baadhi ya matatizo yaliyobainishwa na kupewa kipaumbele yanahusiana na huduma zinazotolewa na serikali, nyenzo hii inaweza kutumika; kukusanya ithibati kuhusu kukithiri kwa tatizo, kuhamasisha jamii kuhusu tatizo, na hata kutafuta majibu kutoka kwa wanaosimamia suala hilo ili kupata suluhu.

Zifutazo ni baadhi ya mbinu za CCT na mapendekezo ya mahali ambako nyenzo hii inaweza kutumika:

| Mbinu ya CCT | Uhamasishaji wa Kanisa na Jamii | Umoja/Parivartan/Unidos | Sangsangai |
|---|---|---|---|
| Wakati wa kutanguliza uandishi wa habari wa raia | **Hatua ya 2:** Maelezo kuhusu kanisa na jamii<br><br>**Hatua ya 3:** Kukusanya taarifa<br><br>**Hatua ya 4:** Uchambuzi wa taarifa<br><br>**Hatua ya 5:** Kufanya Uamuzi | **Hatua ya 2:** Mustakabali wa jamii<br><br>**Hatua ya 3:** Kuweka malengo na kuchukua hatua (kupanga utekelezaji)<br><br>**Hatua ya 4:** Kutekeleza | **Awamu ya 3:** Jamii |

Kanisa na jamii zinaweza kupokea mafunzo kuhusu uandishi wa habari wa raia kupitia nyenzo zilizo hapa chini.

## Kutumia nyenzo

Pana mwongozo wa uandishi wa habari wa raia mwishoni mwa nyenzo hii.

**Ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilisha kulingana na hali iliyopo, tafadhali tembelea learn.tearfund.org/sa-tools**

Hatua muhimu katika uandishi wa habari wa raia:[30]

1. **Chagua suala mahususi kati ya masuala ya kijamii yaliyobainishwa kupitia CCT.** Hii itahakikisha makala yanaungwa mkono na wanajamii, na wanahabari wa raia wanalindwa (rejelea sehemu ya usalama wa kimwili na kidijitali katika 'mapungufu' yaliyoorodheshwa hapo juu).
2. **Fanya utafiti na ufahamu vyema kuhusu haki zako kama mwandishi wa habari wa raia:** Maswali muhimu ya kujiuliza unapowazia kutumia nyenzo hiki ni:
   a. Je,  kuna sheria kuhusu haki ya kupata taarifa?
   b. Je, kuna sheria zingine zozote zinazoweza kusaidia kukusanya taarifa tunazohitaji katika muundo tunaotaka kama vile kurekodi video?

[30]Inarejelea Mare na wenzake (2018)

3. Kuwa mwandishi wa habari wa raia anayewajibika kwa kuzingatia
kanuni za maadili:
    a. Kuripoti kwa usahihi.
    b. Kuepuka kunakili kazi za wengine.
    c. Kuheshimu haki ya usiri.
    d. Kuelewa mambo nyeti yanayohusiana na jamii au watu wanaohusika.
    e. Kuomba idhini zinazohitajika (km kurekodi video au kunasa sauti, kupiga picha, kutumia majina au maelezo mengine ya utambulisho).
4. Panga simulizi yako:
    a. Ni nini kinachoendelea/kilichotokea?
    b. Nani, wapi, na lini?
    c. Kwa nini tukio linatendeka/lilitendeka?
    d. Linawaathiri vipi watu na kwa nini hii ni muhimu?
    e. Ni lipi lipaswa kufanyika kwa sasa?
    f. Nani wanaweza kusaidia kushughulikia tatizo na je, wanafahamu kuwa kuna tatizo?
5. Wazia njia bunifu za kusambaza taarifa (angalia mifano kwenye mwongozo).

## Ufaafu wa nyenzo hii
# Mfano

Shirika la Alliance for Community Action (ACA) nchini Zambia,[31] lina maono kuwa ipo siku ambapo 'wananchi wote wa Zambia watanufaika kikamilifu na kwa usawa kutokana na rasilimali za nchi yao'. Matumaini yao ni kufanikisha hili kwa kuweka mikakati maalum na ya kawaida ya kuwezesha wananchi kufuatilia matumizi ya rasilimali za umma nchini Zambia. Mojawapo ya mikakati wanayotumia kutimiza hili ni kwa kutoa mafunzo ya uanahabari wa raia kwa vijana ambao wanaweza kuhoji watu wanaowajibika kuhusu matumizi ya rasilimali za umma. Waandishi wa habari wa raia hutumia simu za mkononi kuandaa maudhui yaliyo tayari kwa matangazo na usambazaji bila kuhitaji kuhaririwa kwenye kompyuta au studio. Simulizi hizo hupeperushwa hewani kwenye vituo vya redio vya mashinani vinavyoshirikiana na ACA, na pia kwenye mitandao ya kijamii ya ACA.

Huu hapa mfano wa taarifa ya habari iliyotayarishwa na kijana ambaye ni mwanahabari wa raia aliyepokea mafunzo kutoka kwa ACA chini ya mpango wa Speak Up Youth

**Tazama mtandaoni**

[31] Shirika la Alliance for Community Action

# Mwongozo zaidi

Unapopanga kusaidia kanisa na jamii mahususi kutumia nyenzo hii, unahitaji kukusanya habari ili uelewe mambo muhimu ya kijamii na kisiasa ya eneo husika na ubaini ikiwa wanaruhusu matumizi ya nyenzo ya aina hii.

Kusanya habari kuhusu hali ilivyo kuhusiana na masuala ya uanahabari kwenye jamii hiyo:

- Je, kuna sheria kuhusu haki ya kupata taarifa? Au kuna sheria zingine zozote zinazoruhusu kurekodi taarifa?
- Je, kuna kituo cha redio cha jamii?
- Je, kituo cha redio cha jamii kiko tayari kushirikiana na wanahabari wa raia kuandaa simulizi?
- Je, wako tayari kuendesha baadhi ya vipindi vya mafunzo ili kuwafundisha wanahabari wa raia?
- Pawe na wanahabari tofauti wa raia ili uwe na watu wanaoweza kusoma na kuandika katika lugha za wenyeji na pia katika lugha rasmi.

## Viungo vya hati na nyenzo zaidi zinazohusiana na uandishi wa habari wa raia

a. Mwongozo wa kushiriki: Mwanahabari wa raia

b. Mafunzo Binafsi kwa Wanahabari wa Umma

c. Uandishi wa habari wa raia

d. Mwongozo kuhusu Uandishi wa Habari wa Raia

e. Mafunzo kuhusu uanahabari: Wanahabari wa raia

f. Mwongozo kuhusu utetezi na uwajibikaji wa kijamii

g. Mwongozo kuhusu uanahabari wa mashinani

h. Uandishi wa habari wa raia : desturi, uvumi, elimu

i. Wanahabari wa raia wa kike kutoka Zambia

## Faharasa

**Bajeti:** Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi fulani.

**Mwananchi:** Mwenyeji wa nchi fulani, aliye chini ya mamlaka ya taifa hilo, na ambaye ana haki kulindwa na serikali kwa kuwa yeye ni mzaliwa wa huko au amepewa haki hizo.

**Maendeleo yanayosimamiwa na jamii:** Mchakato ambapo wanajamii hushirikiana ili kuchukua hatua za pamoja na kupata suluhu kwa matatizo yanayowakabili.

**Serikali:** Ofisi, idara, na makundi ya watu wanaoendesha nchi, jimbo, jiji, au asasi nyingine ya kisiasa.

**Uanahabari:** Kazi ya kukusanya, kuandika, na kuchapisha habari na makala kwa ajili ya matangazo katika vituo vya habari.

**Kunakili kazi za wengine:** Kuchukua kazi au maudhui ya mtu mwingine kisha kuzimiliki kana kwamba ni zako

**Mpango:** Maamuzi kuhusu jinsi ya kutekeleza mambo fulani siku za mbeleni.

**Sera ya umma:** Sera ya umma ni hatua inayochukuliwa na kuidhinishwa na serikali ili kufikia malengo fulani. Hii inaweza kufanyika kwa njia nyingi. Kwa mfano, inaweza kuwa sheria, mkakati au mpango. Hata hotuba ya rais au waziri inaweza kuelezea mpango wa serikali.

**Mitandao ya kijamii:** Teknolojia shirikishi inayowezesha watumiaji kuunda na kushiriki habari, mawazo, mambo yanayowavutia, na njia zingine za kujieleza kupitia vikundi na miunganisho.

**Vyombo vya habari vya kawaida:** Njia za uanahabari zilizoanzia kabla ya uvumbuzi wa intaneti, ikiwemo magazeti, redio, na televisheni.

# Sampuli ya mwongozo

## Mwongozo wa makala ya mwanahabari wa raia

| Nchi | Tarehe |
|---|---|
| | |
| **Jina la utawala la eneo husika** | |
| | |
| **Jina la jamii/kijiji** | |
| | |
| **Tukio linaloripotiwa** | |
| | |
| **Ripoti imewasilishwa na** | |
| | |
| **Idhini zinazohitajika zimetolewa** | |
| ☐ **Ndiyo**<br>☐ **La** | |

| Kupanga simulizi | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Maswali muhimu | Je, ninajua nini tayari? | Je, ni nani anayeweza kujibu maswali yangu? (Vyanzo va habari) | Majibu | Je, umechukua hatua zipi kuthibitisha habari? |
| **1.** Ni nini kinachoendelea/kilichotokea? | | | | |
| **2.** Nani, wapi na lini? | | | | |
| **3.** Kwa nini tukio linatendeka/lilitendeka? | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **4. Linawaathiri vipi watu na kwa nini hii ni muhimu?** | | | | |
| **5. Ni lipi lipaswa kufanyika kwa sasa?** | | | | |
| **6. Nani wanaweza kusaidia kushughulikia tatizo na je, wanafahamu kuwa kuna tatizo?** | | | | |

<table>
<tr><th colspan="7">Je, ni njia ipi bora zaidi ya kushiriki habari zilizokusanywa?</th></tr>
<tr><td>1. Je, muundo wa maudhui ni upi?</td><td>Video</td><td>Sauti</td><td>Picha</td><td>Makala</td><td>Vibonzo</td><td>Nyingine</td></tr>
<tr><td>2. Je, maudhui yatashirikiwa vipi?</td><td>Mtandaoni<br><br>(k.m mitandao ya kijamii)</td><td>Redio</td><td>Televisheni</td><td colspan="2">Machapisho</td><td>Nyingine</td></tr>
</table>

**Tembelea learn.tearfund.org/sa-tools ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilisha kulingana na hali iliyopo.**

# Nyenzo ya kadi ya tathmini ya jamii



**Jean Bosco Sindayihebura, sehemu ya Dayosisi ya Matana, anarekodi habari kuhusu hali ya afya na lishe ya wanakijiji wa huko Songa.** Picha: Tom Price/Tearfund

## Katika sehemu hii

Kuhusu nyenzo hii • Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha • Mwongozo zaidi •Mfano wa utaratibu • Utaratibu unaoweza kubadilishwa



tearfund

# Kuhusu nyenzo hii[32]

**Kadi ya tathmini ya jamii ni nyenzo ya uwajibikaji ya kijamii inayotumika na wanajamii wenyewe kufuatilia na kutathmini huduma, miradi na hata vitengo vya utawala vya serikali (km ofisi za wilaya).**

## Madhumuni ya nyenzo hii

Kudumisha uwazi, ufanisi na ubora katika utoaji wa huduma za umma kwa wanajamii. Nyenzo hii inalenga kufanikisha hili kwa kuwezesha:

1. kufuatilia huduma zinazopatikana
2. kufuatilia ubora wa huduma au miradi
3. kulinganisha utendakazi katika vituo au wilaya tofauti
4. kuweka utaratibu wa kutuma majibu moja kwa moja kati ya wanaotoa huduma na watumiaji
5. Kukuza uwezo wa wananchi
6. kuimarisha mchango wa wananchi na ustawi wa jamii

Nyenzo hii imeundwa ili itumike mashinani, hasa ufuatiliaji wa vituo maalum, k.m. kliniki, shule au makampuni ya huduma.

[32]Imerejelea Mwongozo wa Uwajibikaji wa Kijamiiwa Evangelical Fellowship of Zimbabwe.

## Ufaafu na upungufu wa nyenzo hii

### Ufaafu

- **Huhimiza mapatano** kupitia mazungumzo ya moja kwa moja kati ya wananchi na watoa huduma.
- **Huimarisha uwajibikaji** wa pamoja kati ya wananchi na watoa huduma, kwa kuwa wananchi huchangia zaidi katika mchakato shirikishi ili kutoa huduma bora na faafu.
- **Hurahisisha usimamizi** wa miradi ya umma.
- **Ni rahisi kutumia** na inafaa kwingi.

### Upungufu

- Maafisa wa serikali za mashinani **huenda wakazuia wananchi kushiriki** na wanaweza kutishiwa na maoni ya raia.
- Maafisa wa serikali za mashinani **huenda wasiwe na uwezo** wa kutosha kutekeleza maoni ya wananchi.
- **Inahitaji mwelekezi bora kati** ya raia na serikali za mashinani ili kuhakikisha wadau wote wanashiriki kikamilifu na migogoro inatatuliwa kwa amani.
- **Inaweza kusababisha matarajio makubwa yasiyowezekana.**

# Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha

## Je, nyenzo hii inatumika katika hatua gani ya mchakato wa CCT?

Michakato tofauti ya CCT hutumika katika mazingira mbalimbali. Nyenzo hii ni mwafaka zaidi baada ya kanisa na wanajamii kutathmini mahitaji yao, kubainisha matatizo yanayowakabili na fursa zilizopo katika jamii zao, na wameanza kukusanya rasilimali ili kushughulikia matatizo hayo. Jumuiya tayari inapitia mabadiliko ya mawazo, ikitambua wakala wao wenyewe. Wanajamii tayari wana mtazamo mpya na wanatambua nafasi yao.

Iwapo baadhi ya matatizo yaliyobainishwa na kupewa kipaumbele yanahusiana na huduma zinazotolewa  na serikali, nyenzo hii inaweza kutumika kukusanya ithibati kuhusu kukithiri kwa tatizo, na inaweza kutumika kwenye mikutano inayohusisha kituo au taasisi husika ya serikali. Wananchi ndio hupata huduma za umma na wako katika nafasi nzuri ya kutoa maoni yao kuhusu ubora wa huduma wanazopokea na kuchangia kuhusu jinsi maboresho na mabadiliko yanavyoweza kufanywa mashinani na kitaifa kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Zifutazo ni baadhi ya mbinu za CCT na mapendekezo ya mahali ambako nyenzo hii inaweza kutumika:

| Mbinu ya CCT | Uhamasishaji wa Kanisa na Jamii | Umoja/Parivartan/Unidos | Sangsangai |
|---|---|---|---|
| Wakati wa kutanguliza kadi ya tathmini ya jamii | **Hatua ya 3:** Kukusanya taarifa<br><br>**Hatua ya 4:** Uchambuzi wa taarifa<br><br>**Hatua ya 5:** Kufanya Uamuzi | **Hatua ya 3:** Kuweka malengo na kuchukua hatua (kupanga utekelezaji)<br><br>**Hatua ya 4:** Kutekeleza | **Awamu ya 3:** Jamii |

## Kutumia nyenzo[33]

Pana mifano ya utaratibu mwishoni mwa mwongozo huu.

**Ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilishakulingana na hali iliyopo, tafadhali tembelea learn.tearfund.org/sa-tools**



[33]Imerejelea The Community Score Card (CARE Malawi, 2013)

Kuna hatua sita kuu za kutekeleza kadi ya tathmini ya jamii:

### Hatua ya 1: Kupanga na kuanza kujiandaa

Hatua hii hurejelea taarifa kutoka kwenye mchakato wa CCT. Matatizo yamebainishwa na kupewa kipaumbele, na masuala yanayohitaji serikali kuingilia kati yametambuliwa.

Wasaidie wanajamii kutambua masuala/matatizo mahususi yanayowakabili kuhusiana na huduma husika. Kwa mfano, ikiwa tatizo lililotambuliwa kwenye mchakato wa CCT ni 'huduma duni za afya kwenye kliniki', sharti wanajamii wasaidiwe kufafanua hili na waelewe maana ya 'huduma duni za afya'. Tumia zoezi kufafanua mtazamo huu na urejelee sababu wanazotoa. (Taarifa hii itapatikana kwa urahisi ikiwa wanajamii wanaelewa jamii yao vizuri, na ikiwa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa umefanyika kwenye mchakato wa CCT.)

**Mtazamo wa wanajamii kuhusu ubora wa huduma za afya kwenye kliniki yao**[34]

| Nimeridhika kabisa | Nimeridhika | Wastani/ Sina uhakika | Sijaridhika | Sijaridhika hata kidogo |
|---|---|---|---|---|
| ☐ | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ |
| **Sababu** | | | | |
| | | | | |

Tumia taarifa iliyopo kubuni vigezo na kuandaa kadi ya tathmini ya jamii

[34]Inarejelea toleo la Evangelical Fellowship of Zimbabwe la Social Accountability Manual

### Hatua ya 2: Kutumia kadi ya tathmini pamoja na wanajamii

Kadi ya tathmini ya jamiihutolewa kwa wanajamii. Kulingana na suala linaloshughulikiwa, inahimizwa kufanya hivi kupitia vikundi maalum, k.m. wanawake pekee, wanaume pekee, vijana pekee, kwa sababu huenda wamehudumiwa kwa njia tofauti sana. Hivyo ukusanyaji data unapaswa kupangwa. Huu hapa mfano wa kadi ya tathmini ya jamii. Pana fomu unayoweza kubadilisha ili kuendana na hali na muktadha mahususi kwenye learn.tearfund.org/sa-tools.

| Tatizo | Kipaumbele | Sababu |
|---|---|---|
| Kliniki yetu haina dawa siku zote | Juu | Tunaandikiwa dawa kila wakati badala ya kupewa kwa hivyo tumeacha kwenda kwenye kliniki tukiwa wagonjwa. |

| | Alama | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kiashiria** | **Duni sana = 1** | **Duni = 2** | **Sawa = 3** | **Nzuri = 4** | **Nzuri sana = 5** |
| Kupata dawa kwenye kliniki yenu | | | | | |
| **Sababu** | | | | | |
| | | | | | |

## Hatua ya 3: **Kupitia kadi ya tathmini na watoa huduma**

Ili kukuza ushirikiano, mtoa huduma anapaswa awe na fursa ya 'kuelezea upande wake'. Hivyo, anapaswa pia awe na fursa ya kuandaa kadi ya tathmini inayoangazia matatizo kama anavyoyaona. 'Tunatoa huduma gani? 'Changamoto kuu ni zipi? Tunaweza kuboresha vipi?'

Huu chini mfano wa kadi ya tathmini i yenye viashiria vilivyotayarishwa na watoa huduma za afya.

| Tatizo | Kipaumbele | Sababu |
|---|---|---|
| Kliniki yetu haina dawa siku zote | Juu | • Wanajamii hukataa kulipa ada.<br>• Wanajamii husubiri hadi wanapougua vikali ila kliniki ina 'dawa za kutibu dalili ambazo hazijakithiri'.<br>• Idadi ya wanajamii imeongezeka, lakini mgao wa dawa kutoka Wizara ya Afya umesalia vile-vile. |

| | Alama | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiashiria | Duni sana = 1 | Duni =2 | Sawa =3 | Nzuri =4 | Nzuri sana =5 |
| Malipo ya ada | | | | | |
| Kupata huduma za afya mapema | | | | | |
| Mgao wa dawa kutoka Wizara ya Afya | | | | | |
| Sababu | | | | | |
| | | | | | |

## Hatua ya 4: Kujumlisha matokeo

Shirikiana na wakusanyaji data/wawakilishi wa jamii ili kujumlisha data, kufanya uchambuzi na kuandaa ripoti ya matokeo. Kama sehemu ya kudumisha uaminifu na ushirikiano, na kulingana na muktadha, huenda ikawa muhimu kushiriki matokeo muhimu na watoa huduma kabla ya mkutano kufanyika ili wawe tayari.

| | Kikundi lengwa | Kijiji cha 1 alama ya wastani | Kijiji cha 2 alama ya wastani | Kijiji cha 3 alama ya wastani | Alama ya jumla ya wastani kwa kila kikundi | Sababu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiashiria cha 1** | Vijana | | | | | |
| | Wanawake | | | | | |
| | Wanaume | | | | | |
| **Matokeo yaliyojumlishwa kulingana na kijiji** | | | | | | |

### Hatua ya 5: **Mkutano wa pamoja na kubuni mipango**

- Baada ya kujumlisha matokeo, mkutano kati ya watoa huduma na wanajamii huendeshwa na mwelekezi wa kuaminika asiyeegemea upande wowote.
- Mkutano huo unakusudiwa kutoa fursa kwa wahusika kushiriki na kujadiliana kuhusu kadi ya tathmini i na kueleza matokeo ya ukadiriaji.
- Hakikisha wakuu wanaofanya maamuzi muhimu wapo ili kupata majibu papo hapo na kujitolea kuchukua hatua.
- Wezesha uundaji wa mpango wa pamoja kati ya wanajamii na watoa huduma unaoangazia mabadiliko yanayoweza kufanywa papo hapo, katika kipindi kifupi, na katika kipindi kirefu, ikiwa yapo. Hii ni muhimu ili kushughulikia matarajio ya wanajamii.

### Hatua ya 6: **Kutekeleza mpango, kufuatilia na kutathmini (M&E)**

Kwenye mkutano, inapaswa kuwekwa wazi kabisa ni nani atakayewajibikia shughuli zipi na lini zitakamilika.

Ni muhimu kuchukulia mchakato huu kama sehemu ya shughuli zingine zinazofanywa kwenye CCT, hivyo taratibu za ufuatiliaji zinazotumika kwa vipengee vingine zitatumika hapa.

## Ufaafu wa nyenzo hii
# Mfano

**Soma mtandaoni**
[Mabingwa wa jamii]

Viongozi wa makanisa na mabingwa wa jamii nchini Zimbabwe walishirikiana kushughulikia masuala ya usambazaji wa maji, usafi wa mazingira, na usimamizi wa taka katika jamii yao pamoja na maafisa wa serikali za mashinani kupitia mikutano na wanajamii na mashauriano ya bajeti. Baada ya kuhamasishwa kuhusu mahitaji ya watoto wenye ulemavu katika jamii yao, wanajamii na maafisa wa serikali za mashinani walishirikiana ili kuboresha huduma za umma kwa watoto hawa.



**Mabingwa wa jamii wakipokea mafunzo kutoka kwa Evangelical Fellowship of Zimbabwe.**
Picha: Evangelical Fellowship of Zimbabwe

Katika jamii kadhaa nchini Zimbabwe, watu hawakuweza kupata maji safi. Mabomba yao ya maji yalikuwa yameharibika na wengi hawakuweza kumudu kununua maji. Badala yake, ilibidi watembee kuchota maji kwenye mto uliokuwa mbali, na mara nyingi maji hayo yalikuwa
na viini.

Mabingwa wa jamii walihamasisha wanajamii kuhusu haki na majukumu yao. Pia walifuatilia matumizi ya mali ya umma na walitumia zana zingine za uwajibikaji wa kijamii kama vile kadi za tathmini na uandishi wa habari wa raia kukusanya taarifa kuhusu matatizo na wasiwasi wa wenyeji. Viongozi wa kanisa pia walichangia pakubwa katika kuwatia moyo waumini wao kushiriki katika michakato hii ya uwajibikaji wa kijamii.

Baada ya kukusanya data ya kutosha kupitia kadi za tathmini ya jamii, mabingwa wa jamii na viongozi wa kanisa walikutana na maafisa wa serikali za mashinani kujadili masuala ya usafi na usambazaji wa maji katika jamii. Maafisa wa serikali walikuwa tayari kabisa kushirikisha mabingwa wa jamii na viongozi wa kanisa katika mashauriano yao ya bajeti na kufuatilia jinsi wanavyoshughulikia matatizo ya jamii.

Baada ya miezi michache, wanajamii walifurahi kupata tena maji safi kwenye mabomba yao.

# Mwongozo zaidi

Unapopanga kusaidia kanisa na jamii mahususi kupitia nyenzo hii, unahitaji kukusanya habari ili uelewe mambo muhimu ya kijamii na kisiasa ya eneo husika na kuhakikisha jamii imebainisha masuala ya utoaji huduma ambayo wangependa yashughulikiwe. Kusanya habari ili ujue ni nani anawajibika kutoa huduma iliyobainishwa na matarajio ni yepi kuhusiana na utoaji huduma.

Tenga muda kuwazia mapema kuhusu utetezi na hatua zinazohitajika kuchukuliwa ili kutimiza ahadi zilizotolewa za kuboresha utoaji huduma. Hizi hapa nyenzo unazoweza kupitia ili kujifunza zaidi kuhusu nyenzo hii.

## Viungo vya hati na nyenzo zaidi zinazohusiana na kadi za tathmini ya jamii

a. Kuchangia kuunda bajeti, Kadi ya Tathmini ya Jamii, Nyenzo ya Kadi ya Ripoti ya Umma, IEA, 2015, uk.42

b. Hatua za kutekeleza Kadi ya Tathmini ya Jamii

c. Mwongozo kuhusu Uwajibikaji wa Kijamii

d. Nyenzo kuhusu Utetezi na uwajibikaji wa kijamii

e. Mwongozo kuhusu Uwajibikaji wa Kijamii kwa Mashirika ya Kijamii na Manispaa nchini Palestine

## Faharasa

**Bajeti:** Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi fulani.

**Maendeleo yanayosimamiwa na jamii:** Mchakato ambapo wanajamii hushirikiana ili kuchukua hatua za pamoja na kupata suluhu kwa matatizo yanayowakabili.

**Serikali:** Ofisi, idara, na makundi ya watu wanaoendesha nchi, jimbo, jiji, au asasi nyingine ya kisiasa.

**Mpango:** Maamuzi kuhusu jinsi ya kutekeleza mambo fulani siku za mbeleni.

**Sera ya umma:** Sera ya umma ni hatua inayochukuliwa na kuidhinishwa na serikali ili kufikia malengo fulani. Hii inaweza kufanyika kwa njia nyingi. Kwa mfano, inaweza kuwa sheria, mkakati au mpango. Hata hotuba ya rais au waziri inaweza kuelezea mpango wa serikali.

# Mfano wa utaratibu

## 1. Utaratibu wa kadi ya tathmini ya jamii

| Nchi | Tarehe |
|---|---|
| | |
| Jina la utawala la eneo husika | |
| | |
| Jina la jamii/kijiji | |
| | |
| Kikundi lengwa (k.m wanawake/wanaume/wavulana/wasichana) | |
| | |

| Matatizo yaliyobainishwa | Kiwango cha kipaumbele (chini/wastani/juu) | Sababu |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |

| | Alama | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiashiria | Duni sana = 1 | Duni = 2 | Sawa = 3 | Nzuri = 4 | Nzuri sana = 5 | Sababu |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |

## 2. Utaratibu wa kujumuisha alama

| Nchi | Tarehe |
|---|---|
| | |
| **Jina la utawala la eneo husika** | |
| | |
| **Jina la jamii/kijiji** | |
| | |

| | Kikundi lengwa | Alama ya wastani | Alama ya wastani | Alama ya wastani | Alama ya jumla ya wastani kwa kila kikundi | Sababu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiashiria cha 1** | Vijana | | | | | |
| | Wanawake | | | | | |
| | Wanaume | | | | | |
| **Alama ya jumla ya wastani kwa kila kikundi** | | | | | | |

| | Kikundi lengwa | Alama ya wastani | Alama ya wastani | Alama ya wastani | Alama ya jumla ya wastani kwa kila kikundi | Sababu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiashiria cha 2** | Vijana | | | | | |
| | Wanawake | | | | | |
| | Wanaume | | | | | |
| **Alama ya jumla ya wastani kwa kila kikundi** | | | | | | |

**Tembelea learn.tearfund.org/sa-tools ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilisha kulingana na hali iliyopo.**

# Nyenzo ya uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma



**Washiriki na watoto wao walio na utapiamlo wanahudhuria mradi wa usalama wa chakula na lishe katika kijiji cha Mutaho, nchini Burundi.** Picha: Tom Price/Tearfund

## Katika sehemu hii

Kuhusu nyenzo hii • Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha • Mwongozo zaidi • Mfano wa utaratibu • Utaratibu unaoweza kubadilishwa



tearfund

# Kuhusu nyenzo hii

**Mbinu hii hutumiwa na wananchi kufuatilia mtiririko wa rasilimali za umma (km fedha, vifaa, mitambo, rasilimali watu) kutoka ngazi za juu za serikali, kupitia mfumo ya kiutawala katika ngazi tofauti, hadi watoa huduma za umma walio mstari wa mbele.**

## Madhumuni ya nyenzo hii

Kwa wananchi kutathmini kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli unaoendeshwa na watoa huduma walio kwenye mstari wa mbele. Kubaini kiasi cha fedha ambacho kimetumika, kinatumika na matokeo yaliyowezekana kupitia fedha ambazo tayari zimetumika.

Nyenzo hii inaweza kutumika katika ngazi zote za serikali ambapo mgao na matumizi ya fedha hufanyika.

## Ufaafu na upungufu wa nyenzo hii

### Ufaafu

- Inaweza kutumika kwa ufanisi kufuatilia masuala yanayowakumba wananchi.
- Inawezesha uwajibikaji katika masuala ya mashinani na pia yale ya kimfumo kwa ujumla.
- Inazuia ufisadi na mapungufu katika utoaji wa huduma.

### Upungufu

- Matatizo yanaweza kuibuka ikiwa data haipo, haipatikani, au iko katika muundo usioweza kutumika, iwe kwa makusudi au la.



# Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha

## Je, nyenzo hii inatumika katika hatua gani ya CCT?

Michakato tofauti ya CCT hutumika katika mazingira mbalimbali. Nyenzo hii ni mwafaka zaidi katika hatua ambapo rasilimali zilizopo zimebainishwa: wanajamii, pamoja na kanisa, wamefanya tathmini ya mahitaji yao, wamebaini matatizo na fursa zilizopo katika jamii zao, wameyapa vipaumbele matatizo ambayo wangependa kuangazia, na wameanza kukusanya rasilimali ili kushughulikia matatizo hayo. Ikiwa serikali tayari inaangazia tatizo ambalo limepewa kipaumbele, nyenzo hii inaweza kutumika kuhakikisha tatizo limeshughulikiwa vilivyo kwa kutumia rasilimali zilizopo. Nyenzo hii itasaidia jamii kufuatilia jinsi fedha hizo zinavyotumika.

Zifutazo ni baadhi ya mbinu za CCT na mapendekezo ya mahali ambako nyenzo hii inaweza kutumika:

| Mbinu ya CCT | Uhamasishaji wa Kanisa na Jamii | Umoja/Parivartan/Unidos | Sangsangai |
|---|---|---|---|
| Kuanza kufuatilia matumizi ya fedha za umma | **Hatua ya 4:** Uchambuzi wa taarifa<br><br>**Hatua ya 5:** Kufanya Uamuzi | **Hatua ya 3:** Kuweka malengo na kuchukua hatua (kupanga utekelezaji)<br><br>**Hatua ya 4:** Kutekeleza | **Awamu ya 3:** Jamii |

## Kutumia nyenzo

**Kufanya uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma (PETS)**

Hapa chini pana mfano wa jinsi nyenzo hii imetumika (utaratibu wa 1). Kanisa na wanajamii wanaweza kufanya uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma kwa kutumia nyenzo mpya (utaratibu wa 2).

**Ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilishakulingana na hali iliyopo, tafadhali tembelea learn.tearfund.org/sa-tools**

Zifuatazo ni hatua muhimu za kuchukua katika kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwa kutumia nyenzo hii.

1. Unda timu ya PETS: Ikiwezekana, wanachama wanapaswa kuteuliwa na wanajamii. Idadi ya wanachama hutofautiana, lakini kawaida huwa kati ya tisa na 14. Inapaswa kujumuisha wanawake na wanaume, na watu wa umri, kabila na hadhi tofauti kwenye jamii.

2. Kufanya utafiti: Fahamu sheria na sera zilizopo katika nchi yako zinazohusiana na uwazi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mfano, kunaweza kuwa na sheria zinazoruhusu wananchi kufikia taarifa kuhusu matumizi ya fedha za umma.

3. Kujenga mahusiano: Ni muhimu sana kujenga uhusiano na watu katika idara husika ya serikali au mamlaka ya mitaa, na viongozi wa jamii.
4. Kubaliana kuhusu suala/mradi wa kufuatilia kulingana na vipaumbele vilivyobainishwa kwenye mchakato wa kutambua tatizo na kuweka vipaumbele wa CCT.
5. Kusanya taarifa unazohitaji kuhusu matumizi ya fedha za umma. Jaribu kupata taarifa unazohitaji kuhusu mipango, bajeti na matumizi ya fedha ya serikali za mitaa. Baada ya kupata stakabadhi zote, zisome kwa makini. Usijali ikiwa una maswali kuhusu mambo ambayo huelewi – unaweza kuwauliza wahudumu ofisini au maafisa wa mamlaka waliokupa bajeti hiyo.
6. Kujua kinachoendelea: Je, fedha za mradi zinatumika inavyofaa?
7. Chambua taarifa zote – je, ukijumlisha fedha zote, kuna uwiano wa kiasi kilichotengwa, kiasi kilichotumika na maendeleo yaliyopatikana?
8. Majibu kwa wanajamii na wale wanaohusika na bajeti na matumizi yake, kisha uamue jinsi ya kufuatilia. Kusanya taarifa zote, changanua, andika ripoti kisha ufanye mkutano na wanajamii ili kuhakikisha kila mtu ana fursa ya kusikia matokeo uliyopata, na kuhusika katika ufuatiliaji wowote utakaohitajika.

## Ufaafu wa nyenzo hii

# Mfano

**Soma mtandaoni**

[Utetezi nchini Uganda: Kujenga uhusiano na serikali za mitaa]

Kupitia mafunzo kuhusu ustawi wa kanisa na jamii nchini Uganda, kanisa la mashinani liliunga mkono kijiji chao kushinikiza serikali ya mtaa kutoa huduma za afya walizohitaji sana, licha ya kuwa serikali ilikuwa imesitasita. Kupitia usaidizi wa kanisa hilo, wanakijiji walishirikiana na maafisa wa serikali yao ya mashinani kufuatilia matumizi ya fedha za umma, hivyo kuimarisha uwajibikaji wa serikali ya kitaifa na ya mashinani. Kwa pamoja, walihakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya huduma za afya za umma zinafikia jamii kwa ufanisi.

# Mwongozo zaidi

Unapopanga kutumia nyenzo hii kusaidia kanisa na jamii katika eneo fulani, unahitaji kukusanya habari ili uelewe mambo muhimu kuhusu mipango yao ya matumizi ya fedha kitaifa na kieneo ili uwe na ujasiri kwa suala hilo.
Kisha fanya hivyo kwa kushirikisha wanajamii ili kwa pamoja mpate kuelewa kwa kina kuhusu matumizi ya fedha mashinani.

Maswali muhimu ya kuangaziwa:

1. Je, nchini bajeti hupitishwa lini kieneo na kitaifa?
2. Ni aina gani ya serikali iliyopo? Je, ni serikali kuu au ya ugatuzi?
3. Ni rasilimali gani hutumwa mashinani, lini, mara ngapi?
4. Ni njia zipi zilizopo za kupata taarifa kuhusu matumizi ya fedha?
5. Je, tarehe zipi muhimu katika utoaji fedha, matumizi na kuripoti?

## Kiungo cha hati kuhusu kufuatilia matumizi ya fedha za umma

Mwongozo wa kina kuhusu PETS

## Faharasa

**Ukaguzi wa hesabu:** Ukaguzi rasmi wa fedha za shirika, kawaida hufanywa na kampuni huru.

**Bajeti:** Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi fulani.

**Kutumia utawala mkuu:** Kuunda mfumo ambapo kundi moja kuu la watu hutawala vikundi vya kieneo.

**Mwananchi:** Mwenyeji wa nchi fulani, aliye chini ya mamlaka ya taifa hilo, na ambaye ana haki kulindwa na serikali kwa kuwa yeye ni mzaliwa wa huko au amepewa haki hizo.

**Maendeleo yanayosimamiwa na jamii:** Mchakato ambapo wanajamii hushirikiana ili kuchukua hatua za pamoja na kupata suluhu kwa matatizo yanayowakabili.

**Ufisadi:** Tabia ya ulaghai au ukosefu wa uaminifu kwa walio madarakani, kaiwaida huhusisha rushwa.

**Ugavi:** Utoaji pesa kutoka kwenye hazina.

**Mchakato wa matumizi ya fedha:** Shughuli zinazohusiana na ununuzi na malipo ya bidhaa na huduma. Shughuli hizi zinahusisha uamuzi wa kile kinachohitaji kununuliwa, shughuli za ununuzi, upokeaji wa bidhaa, na malipo kwa wauzaji.

**Mwaka wa fedha:** Kipindi cha miezi kumi na miwili (sio lazima iwe tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba) ambapo serikali au biashara hupanga bajeti.

**Serikali:** Ofisi, idara, na makundi ya watu wanaoendesha nchi, jimbo, jiji, au asasi nyingine ya kisiasa.

**Mpango:** Maamuzi kuhusu jinsi ya kutekeleza mambo fulani siku za mbeleni.

**Sera ya umma:** Sera ya umma ni hatua inayochukuliwa na kuidhinishwa na serikali ili kufikia malengo fulani. Hii inaweza kufanyika kwa njia nyingi. Kwa mfano, inaweza kuwa sheria, mkakati au mpango. Hata hotuba ya rais au waziri inaweza kuelezea mpango wa serikali.

**Utumishi wa umma:** Huduma inayohusika na utawala wa umma wa serikali ya nchi. Haijumuishi bunge, mahakama, na vitengo vya kijeshi. Watumishi wa umma hawana wajibu wa kushiriki katika mirengo ya kisiasa, na kijumla hawaathiriwi na mabadiliko ya serikali. Shughuli za kusambaza bidhaa muhimu, kama vile gesi au umeme, au huduma, kama vile usafiri wa umma, kwa umma kwa ujumla, kwa malipo au bila malipo.

## 1. Nyenzo ya uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma(PETS) – mfano[35]

| Maelezo ya mtumiaji | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Jina/kikundi** | *Mustafa G.* | | | |
| **Jinsia** | Mwanamme: | ✔ | Mwanamke: | |
| **Umri/miaka ya kuhudumu** | | | | |
| **Shirika/<br><br>kategoria** | *Kamati inayosimamia mradi* | | | |
| **Kaunti ndogo anakoishi** | *Kaunti Ndogo ya Kufikia Kusini* | | | |
| **Wadi anakoishi** | *Wadi ya Kushiriki* | | | |

| Sekta inayofanyiwa tathmini | |
|---|---|
| Afya | |
| **Eneo linalofanyiwa tathmini** | **Jina** |
| **Kaunti ndogo** | *Kaunti Ndogo ya Kufikia Mashariki* |
| **Wadi** | *Wadi ya Kushiriki* |
| **Kijiji** | *Mafanikio* |

[35]Imerejelea Nyenzo ya *GAF ya Uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma*: *Nyenzo ya Kaunti*

| Tarehe ya Utafiti |
|---|
| 12 Desemba 2018 |

## Mwaka wa Fedha wa Utekelezaji wa mradi 2017/2018

| Maelezo kuhusu mradi na aina ya utekelezaji |
|---|
| *Ujenzi wa Kituo kipya cha Afya huko Mafanikio* |
| **Kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti** |
| *3,000,000* |
| **Kiasi kilichotolewa** |
| *5,217,419* |
| **Kiasi kilichotumika** |
| *? haijulikani* |
| **Tofauti** |
| *?* |
| **Hatua ya utekelezaji** |
| *Haijakamilika* |
| **Maoni ya wanajamii** |
| *Ujenzi ulifikia hatua ya kuezeka paa, lakini wakandarasi waliacha kuja kazini na jengo limesalia hivyo bila kukamilika kwa miezi kadhaa.* |

## Maswali ya utafiti yanayohusiana na ubora – mfano

| La. | Ufafanuzi | Ndiyo | La | Ufafanuzi wa kina |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Je, wanajamii walihusika katika kuchagua mradi huu? | ✔ | | *Ndiyo, wanajamii walitamani mradi huu kwa muda mrefu.* |
| 2 | Je, wanajamii wameridhika na eneo la mradi? | ✔ | | *Ndiyo, eneo lililochaguliwa linafaa.* |
| 3 | Umeona michoro ya ujenzi ya mradi huu? | | ✔ | *Michoro hiyo haikutolewa kwa kamati inayosimamia mradi.* |
| 4 | Jina la kampuni iliyopewa kandarasi/zabuni | | | *M/S Koi-Mag General Constructors Ltd* |
| 5 | Je, kamati ya maendeleo ya wadi ilihusika katika kutoa zabuni/kandarasi? | | ✔ | |
| 6 | Je, kumekuwepo na malalamishi kuhusu uadilifu wa mkandarasi? | ✔ | | *Mkandarasi amesitisha ujenzi na mradi umekwama.* |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **7** | **Ikiwa kulikuwepo na malalamiko yoyote kuhusu mradi, je yaliwasilishwa?** | ✔ | | *Ndiyo, Mamlaka ya Kaunti ya Mafanikio (MCA) imepokea ripoti kuhusu kutoweka kwa mkandarasi, na kufikia sasa hakuna hatua imechukuliwa.* |
| **8** | **Je, mradi umefikia hatua sawia na ilivyoratibiwa?** | | ✔ | *Tarehe ya kukamilika kwa mradi ilikuwa Juni 13, 2018. Tuko Desemba 2018 na mradi umekwama 60%.* |
| **9** | **Ikiwa mradi haujakamilika, unajua sababu?** | | ✔ | *Hapana, mkandarasi hakuji tena kwenye eneo la ujenzi na haijulikani kwa nini ujenzi umesimama.* |
| **10** | **Kadiria utekelezaji wa mradi kwa vipimo vifuatavyo (teua moja) na ueleze sababu.** | Nzuri kabisa: | | |
| | | Nzuri: | | |
| | | Duni: ✔ | | *Ujenzi umefikia hatua ya kuezeka paa* |

# 2.Nyenzo ya Uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma (PETS) – utaratibu[36]

| Maelezo ya mhusika | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Jina/kikundi** | | | | |
| **Jinsia** | Mwanamme: | | Mwanamke: | |
| **Umri/miaka ya kuhudumu** | | | | |
| **Shirika/<br><br>Kategoria** | | | | |
| **Kaunti ndogo anakoishi** | | | | |
| **Wadi anakoishi** | | | | |

| Sekta inayofanyiwa tathmini | |
|---|---|
| | |
| **Eneo linalofanyiwa tathmini** | **Jina** |
| **Kaunti ndogo** | |
| **Wadi** | |
| **Kijiji** | |

[36]Imerejelea nyenzo ya *GAF ya Uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma*: *Nyenzo ya Kaunti*

| Tarehe ya Utafiti |
| --- |
| |

## Mwaka wa Fedha wa Utekelezaji wa mradi /

| Maelezo kuhusu mradi na aina ya utekelezaji |
| --- |
| |
| **Kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti** |
| |
| **Kiasi kilichotolewa** |
| |
| **Kiasi kilichotumika** |
| |
| **Tofauti** |
| |
| **Hatua ya utekelezaji** |
| |
| **Maoni ya wanajamii** |
| |


## Maswali ya utafiti yanayohusiana na ubora

| La. | Ufafanuzi | Ndiyo | La | Ufafanuzi wa kina |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Je, wanajamii walihusika katika kuchagua mradi huu? | | | |
| 2 | Je, wanajamii wameridhika na eneo la mradi? | | | |
| 3 | Umeona michoro ya ujenzi ya mradi huu? | | | |
| 4 | Jina la kampuni iliyopewa kandarasi/zabuni | | | |
| 5 | Je, kamati ya maendeleo ya wadi ilihusika katika kutoa zabuni/kandarasi? | | | |
| 6 | Je, kumekuwepo na malalamishi kuhusu uadilifu wa mkandarasi? | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **7** | **Ikiwa kulikuwepo na malalamiko yoyote kuhusu mradi, je yaliwasilishwa?** | | | |
| **8** | **Je, mradi umefikia hatua sawia na ilivyoratibiwa?** | | | |
| **9** | **Ikiwa mradi haujakamilika, unajua sababu?** | | | |
| **10** | **Kadiria utekelezaji wa mradi kwa vipimo vifuatavyo (teua moja) na ueleze sababu.** | Nzuri kabisa: | | |
| | | Nzuri: | | |
| | | Duni: | | |
| **11** | **Ikiwa ni salama, piga picha ya mradi kisha uiambatishe hapa kama ithibati ya hatua ya utekelezaji wa mradi.** | | | |

**Tembelea learn.tearfund.org/sa-tools ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilisha kulingana na hali iliyopo.**

# Nyenzo ya ukaguzi wa kijamii



Warsha ya kuendeleza amani nchini Kenya, wengi wa waliohudhuria ni waleta-amani kutoka **Sudan Kusini** Picha: Diane Igirimbabazi/Tearfund

## Katika sehemu hii

Kuhusu nyenzo hii • Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha • Mwongozo zaidi • Mfano wa utaratibu • Utaratibu unaoweza kubadilishwa

# Kuhusu nyenzo hii

**Nyenzo hii haipaswi kuchukuliwa kuwa ukaguzi wa fedha au utendakazi. Pia ina wigo mpana zaidi kuliko kadi za ripoti za umma au kadi za tathmini ya jamii Ukaguzi wa kijamii hukusanya ithibati kutoka kwa wadau mbalimbali ili kutoa taarifa sahihi katika hatua zote za utekelezaji wa sera za serikali, ikiwemo usimamizi wa fedha, upatikanaji wa taarifa, na ushiriki.**

## Madhumuni ya nyenzo hii

Kutoa taarifa sahihi kwa watoa huduma na wanajamii kuhusu kiwango cha mafanikio na yanayohitaji kuboreshwa katika utoaji huduma. Nyenzo hii inasaidia kuzuia ufisadi kwa:

- kuifichua
- kuhamasisha wanajamii kuhusu jinsi sera za umma zinavyowaathiri
- kuhimiza wananchi kutoa maoni yao kuhusu mahitaji yao na kushinikiza serikali
- kutathmini uwiano wa kati ya sera au ahadi zinazotolewa na serikali na matokeo

Nyenzo hii inaweza kutumika katika ngazi zote za serikali. Inaweza kuanzia kwa mradi maalum mashinani, hadi kwa idara ya serikali, au mipango kadhaa ya kitaifa.

## Ufaafu na upungufu wa nyenzo hii

### Ufaafu

- Huhamasisha umma kuhusu sera, mipango na miradi ya serikali na kudhihirisha jinsi yote haya yanavyowaathiri.
- Hufafanua umuhimu na athari za sera na mipango ya serikali.
- Hudumisha uwazi na ufanisi wa serikali katika kutoa mipango na kutekeleza sera.

### Upungufu

- Inahitaji wadau wote wawe tayari kuhusika katika awamu zote za mchakato.
- Ni faafu zaidi ikiwa kuna sheria kuhusu haki ya kupata taarifa.

# Kutumia na kutekeleza nyenzo kulingana na muktadha

## Je, nyenzo hii inatumika katika hatua gani ya mchakato wa CCT?

Michakato tofauti ya CCT hutumika katika mazingira mbalimbali. Nyenzo hii ni mwafaka zaidi katika hatua ambapo rasilimali zilizopo zimebainishwa: wanajamii, pamoja na kanisa, wamefanya tathmini ya mahitaji yao, wamebaini matatizo na fursa zilizopo katika jamii zao, wameyapa vipaumbele matatizo ambayo wangependa kuangazia, na wameanza kukusanya rasilimali ili kushughulikia matatizo hayo. Ikiwa serikali tayari inatekeleza mradi wa kushughulikia tatizo lililotambuliwa na kupewa kipaumbele na wanajamii, nyenzo hii inaweza kutumika kuhakikisha tatizo linashughulikiwa kwa njia bora zaidi ili kupata suluhu iliyokusudiwa. Nyenzo hii itasaidia jamii kubaini ikiwa shughuli, miradi au mipango inaleta suluhu.

Zifutazo ni baadhi ya mbinu za CCT na mapendekezo ya mahali ambako nyenzo hii inaweza kutumika:

| Utaratibu wa CCT | Uhamasishaji wa Kanisa na Jamii | Umoja/Parivartan/Unidos | Sangsangai |
|---|---|---|---|
| **Kuanza ukaguzi wa kijamii kwenye mchakato.** | **Hatua ya 4:** Uchambuzi wa taarifa<br><br>**Hatua ya 5:** Kufanya Uamuzi | **Hatua ya 3:** Kuweka malengo na kuchukua hatua (kupanga utekelezaji)<br><br>**Hatua ya 4:** Kutekeleza<br><br>**Hatua ya 5:** Tathmini | **Awamu ya 3:** Jamii |

## Kutumia nyenzo

Kanisa na wanajamii wanaweza kufunzwa jinsi ya kuendesha ukaguzi wa kijamii kwa kutumia nyenzo madhubuti kama vile ukaguzi wa kijamii. Pana mfano wa utaratibu mwishoni mwa mwongozo huu.

**Ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilishakulingana na hali iliyopo, tafadhali tembelea learn.tearfund.org/sa-tools**

Hatua muhimu kwenye mchakato wa ukaguzi wa kijamii:

### Hatua ya 1: Kutambua tatizo

Hatua ya kwanza ni kutambua matatizo mahususi yanayowakumba wanajamii katika mwingiliano wao na utumishi/mamlaka ya umma kama ilivyoangaziwa na kupewa kipaumbele wakati wa uchanganuzi wa matatizo kwenye mchakato wa CCT.

### Hatua ya 2: **Kubainisha taarifa muhimu**

Hii ni rahisi zaidi ikiwa nchi ina sheria kuhusu haki ya kupata taarifa (RTI) au desturi ya kukusanya data wazi - hii ni muhimu katika kuchangia kuunda bajeti na uwajibikaji. Sheria na taratibu ambazo maafisa wa umma sharti wazingatie, na data inayohusiana na matatizo maalum ambayo yanahitaji kushughulikiwa, sharti zizingatiwe wakati wa kukusanya taarifa.

- Bajeti, mipango na sera za ufikiaji: Ukaguzi wa kijamii ni nyenzo ya kulinganisha jinsi mpango au huduma ya serikali ulivyo ikilinganishwa na jinsi inavyopaswa kufanya kazi kulingana na malengo, bajeti, stakabadhi, sera na ripoti za mradi/serikali.
- Linganisha matumizi halisi ya fedha na bajeti.
- Tathmini ubora na hali ya huduma/mipango ya serikali.

### Hatua ya 3: **Kutafuta taarifa**

- Angalia ikiwa taarifa sahihi inatayarishwa, na nani, na zinapatikana wapi.
- Andaa maswali ya kuongoza tathmini ya umma. Ili kukusanya taarifa sahihi, washiriki sharti waandae maswali ambayo yatawapa majibu wanayotafuta kuhusu mpango/huduma wanayokagua. Hili limebainishwa katika nyenzo ya ukaguzi wa kijamii, hapa chini.

- Wafunze washiriki, wakazi na/au wanajamii kuhusu mbinu hizo. Zoezi hili hufanywa na makundi makubwa ya watu/wakazi, na ni muhimu kuwapa mafunzo. Washiriki wamefunzwa ili kuwasaidia:

  **a.** Kuelewa sera za serikali na hati za bajeti.

  **b.** Kujifunza kukusanya na kufasiri taarifa wakati wa ukaguzi.

  **c.** Kufasiri taarifa na kuandaa maswali.

### Hatua ya 4: Kupata taarifa

Hatua inayofuata ni kupata taarifa zinazohitajika au zilizobainishwa. Katika nchi kadhaa, maelezo kuhusu utendakazi wa mashirika ya umma ni ya usiri sana.

1. Tambua na uchanganue stakabadhi husika kwa utaratibu na uhakikishe umepata nakala zilizothibitishwa za stakabadhi hizo.
2. Kagua stakabadhi ili uweze kutambua pengo kati ya kiasi kilichopangwa kwenye bajeti na kile kilichotumika. Ukaguzi utaangazia maswali yafuatayo: 'Je, pesa zimetumika ipasavyo katika bajeti?' 'Je, hii ndiyo bidhaa bora zaidi tunayoweza kupata kwa kiasi hiki cha pesa?'
3. Ukaguzi utahitaji watu wenye ujuzi wa kitaaluma na wanaofahamu masuala ya eneo lao.

## Hatua ya 5: **Kupekua taarifa**

1. Kusanya na urahisishe taarifa katika muundo unaoweza kutumika kabla ya watu binafsi na wanajamii kupitia hati hizo. Baadhi ya wananchi huenda wasiwe na ujuzi wa kitaaluma wa kuelewa hati halisi. Katika hatua hii, taarifa changamano zinazopatikana kupitia rekodi za mradi zinastahili kufupishwa katika muundo rahisi.
    - Thibitisha taarifa hiyo na wanajamii kwani wao ni vyanzo muhimu vya taarifa hiyo.
    - Wachunguzi wa nyanjani sharti tayari wawe na ujuzi kamili kuhusu suala, matatizo husika, na udanganyifu uliopo katika visa vya ufisadi.

## Hatua ya 6: **Kukagua taarifa**

Hatua hii inahusisha ukaguzi wa taarifa ili kushughulikia malalamishi.


Baada ya kupata ushahidi kuhusiana na tukio la ufisadi, jitihada hufanywa ili kutatua tatizo na kushughulikia malalamishi ya umma. Chaguo mbili zilizopo ni:

1. Kutumia mbinu za kitaasisi zilizopo za kushughulikia malalamishi kwa kutumia stakabadhi husika.
2. Wananchi wanaweza kushiriki katika mabaraza ya kisheria ili kuwezesha ukaguzi huo.

## Hatua ya 7: **Kufanya mkutano wa hadhara**

Hii ndiyo hatua muhimu zaidi ya ukaguzi wa kijamii, kwani hapa ndipo upekuzi wa pamoja hufanyika. Ni kilele cha mchakato wa ukaguzi wa kijamii.

- Mkutano wa hadhara unahitaji kuendeshwa na mwelekezi asiyeegemea upande wowote.
- Lengo si kuwaaibisha watu hadharani, bali kuhimiza utoaji wa huduma bora.
- Washiriki au timu ya ukagizi wa kijamii huwasilisha matokeo yao kwa mamlaka za mitaa na kwa wanajamii kwa ujumla. Mikutano hii ya hadhara huwapa wanajamii fursa ya kuzungumza kuhusu mpango/huduma inayofanyiwa ukaguzi.
- Mamlaka za mitaa zina fursa ya kusikiliza maoni ya wanajamii ili kubaini fursa za kuboresha huduma.
- Mipango ya utekelezaji huratibiwa ili kushughulikia matatizo yaliyotambuliwa.



## Ufaafu wa nyenzo hii
# Mfano

**Kituo cha nyanjani cha ukuaji na elimu ya chekechea kilikuwa kinajengwa katika kaunti inayopokea usaidizi chini ya mpango wa *Agile and Harmonised Assistance for Devolved Institutions* (AHADI) wa USAID. Jamii ilitaka kuhakikisha kwamba rasilimali hii muhimu inatimiza mahitaji na matarajio yao ya kuimarisha ufikiaji wa elimu bora katika mazingira salama. Hivyo, wanajamii wakafanya ukaguzi wa kijamii.**

Baada ya upekuzi wa kina wa stakabadhi za mradi, wanajamii walikubaliana kwa kauli moja kwamba kulikuwepo na tofauti kubwa kati ya mijengo na ramani za ujenzi. Raia waliwasilisha malalamishi yao kwa Mkurugenzi wa Ukuaji wa Watoto na Elimu ya Chekechea wa Kaunti, na kwa Mjumbe wa Bunge la Kaunti la eneo hilo. Viongozi wa kaunti walimwita mkandarasi afike kwenye mkutano wa hadhara ili kuelezea tofauti hiyo.

Mkandarasi alikubali kusimamia gharama, alibomoa majengo yenye kasoro na kujenga upya kituo cha elimu, akizingatia muundo ulioidhinishwa na vipimo vilivyo kwenye kandarasi. Ujenzi ulikamilika kwa usimamizi wa karibu kutoka kwa Wahandisi wa Ujenzi wa Umma wa Kaunti, na Bodi ya Usimamizi ya shule.[37]

---

[37]Nyenzo ya Kaunti

# Mwongozo zaidi

Kabla ya kuanza kutumia nyenzo ya ukaguzi wa kijamii:

- Hakikisha unaelewa vyema utaratibu wa CCT unaotumika katika jamii ambako utatumia nyenzo hii.
- Kusanya taarifa mapema ukiangazia maswali yafuatayo:
    1. Je, kuna sheria kuhusu haki ya kupata taarifa?
    2. Je, taasisi za serikali ziko tayari kushiriki taarifa? Ikiwa sivyo, utahitaji kuchukua hatua fulani kwa sababu itakuwa vigumu kufanya ukaguzi wa kijamii bila stakabadhi muhimu zinazohusu mradi unaofanyiwa ukaguzi.

## Viungo vya hati na nyenzo kuhusu ukaguzi wa kijamii.

a. Mwongozo kuhusu Uwajibikaji wa Kijamii

b. Nyenzo kuhusu utetezi na uwajibikaji wa kijamii

c. Ukaguzi wa Kijamii: Mwongozo kuhusu Maboresho ya Utendakazi na Kupima Matokeo

d. Mwongozo kuhusu Uwajibikaji wa Kijamii kwa Mashirika ya Kijamii na Manispaa nchini Palestine

e. Mwongozo kuhusu Uwajibikaji wa Kijamii: Dhana na Nyenzo

## Faharasa

**Ukaguzi wa hesabu:** Ukaguzi rasmi wa fedha za shirika, kawaida hufanywa na kampuni huru.

**Bajeti:** Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi fulani.

**Maendeleo yanayosimamiwa na jamii:** Mchakato ambapo wanajamii hushirikiana ili kuchukua hatua za pamoja na kupata suluhu kwa matatizo yanayowakabili.

**Ufisadi:** Tabia ya ulaghai au ukosefu wa uaminifu kwa walio madarakani, kaiwaida huhusisha rushwa.

**Mwaka wa fedha:** Kipindi cha miezi kumi na miwili (sio lazima iwe tarehe 1 Januari hadi tarehe 31 Desemba) ambapo serikali au biashara hupanga bajeti.

**Serikali:** Ofisi, idara, na makundi ya watu wanaoendesha nchi, jimbo, jiji, au asasi nyingine ya kisiasa.

**Mpango:** Maamuzi kuhusu jinsi ya kutekeleza mambo fulani siku za mbeleni.

**Sera ya umma:** Sera ya umma ni hatua inayochukuliwa na kuidhinishwa na serikali ili kufikia malengo fulani. Hii inaweza kufanyika kwa njia nyingi. Kwa mfano, inaweza kuwa sheria, mkakati au mpango. Hata hotuba ya rais au waziri inaweza kuelezea mpango wa serikali.

# Sampuli ya mwongozo

## Nyenzo ya ukaguzi wa kijamii[38]

| **Nchi** | **Tarehe** |
|---|---|
| | |
| **Jina la utawala la eneo husika** | |
| | |
| **Jina la mradi** | |
| | |
| **Mwaka wa fedha** | **Robo** |
| | |
| **Sekta** | |
| | |

[38]Inarejelea Gikonyo (2008)

| A. Ukaguzi wa Kijamii: Maswali tangulizi na yanayohusu usimamizi | | |
|---|---|---|
| **Swali** | **Vyanzo vya taarifa** | **Jibu/maoni** |
| **1.** Je, wanajamii walishiriki katika mchakato wa kuchagua mradi huu? | | |
| **2.** Je, mradi umekusudiwa kushughulikia tatizo/masuala yepi? (Malengo ya kijamii ya miradi ni yapi?) Pitia hati ya mradi au hati za CCT ili upate taarifa hii | | |
| **3.** Je, mamlaka za mitaa zinahusika vipi kisheria katika kusimamia mradi huu? | | |
| **4.** Je, ni hati zipi husika zinahitajika katika kutolewa kwa pesa za mradi? | | |

| | | |
|---|---|---|
| **5. Je, wadau mbalimbali wanahusika vipi katika usimamizi wa mradi (ndani na nje)?** | | |
| **6. Je, mamlaka za mitaa huhifadhi hati zipi muhimu zinazohusiana na usimamizi wa mradi?** | | |
| **7. Je, wakandarasi/wasimamizi wa mradi huhifadhi hati zipi muhimu zinazohusiana na mradi?** | | |
| **8. Ni awamu zipi muhimu ambazo mkandarasi wa mradi sharti akamilishe ili alipwe? (Rejelea mkataba ikiwa unapatikana)** | | |

| | | |
|---|---|---|
| **9.** Ripoti zipi huandaliwa na taasisi mbalimbali katika usimamizi wa mradi? | | |
| **B. Maswali kuhusu manunuzi kwa ajili ya ukaguzi wa kijamii** | | |
| **Swali** | **Vyanzo vya taarifa** | **Jibu/maoni** |
| **1.** Ni hatua gani muhimu za utoaji kandarasi kulingana na miongozo na sheria? | | |
| **2.** Ni mfumo gani wa utoaji kandarasi unaotumika katika usimamizi wa miradi? | | |
| **3.** Miradi hutoa kandarasi vipi katika eneo-bunge lako? | | |
| **4.** Aina tofauti za utoaji kandarasi ni zipi? | | |

| | | |
|---|---|---|
| **5.** **Taja baadhi ya hati muhimu za utoaji kandarasi, ikiwemo hati za lazima za zabuni, zinazohusiana na utoaji kandarasi.** | | |
| **6.** **Je, baadhi ya matukio ya ukiukaji katika utoaji kandarasi ni yepi?** | | |
| **7.** **Toa mapendekezo kuhusu jinsi utoaji kandarasi unavyoweza kuimarishwa kwa kurejelea mapungufu yaliyobainishwa kwenye sehemu ya (6) hapo juu.** | | |

| C. Maswali muhimu ya ukaguzi wa kijamii | | |
|---|---|---|
| **Swali** | **Vyanzo vya taarifa** | **Jibu/maoni** |
| **1. Kwa nini mradi huu umechaguliwa kwa ajili ya ukaguzi wa kijamii kati ya matatizo yaliyopewa kipaumbele kwenye CCT? (Lengo la kijamii)** | | |
| **2. Linganisha shughuli na malengo: Je, shughuli kuu za mradi ni zipi, na je, zinaweza kusaidia kufikia malengo?** | | |
| **3. Je, kuna masharti yepi mahususi ya mradi kulingana na utoaji kandarasi na viwango vilivyowekwa? Je, masharti hayo yametimizwa?** | | |
| **4. Je, pesa zilizotengwa kwa mradi maalum zilifika kwenye mradi?** | | |

| | | |
|---|---|---|
| **5. Je, ubora na vipimo vya vifaa vinavyotumika unalingana na viwango vilivyowekwa? Kumbuka kwamba 'vifaa' vinajumuisha watu. Ikiwa mradi unahitaji wafanyakazi waajiriwe, je, wana ujuzi unaohitajika?** | | |
| **6. Je, wafanyakazi wote walilipwa kama inavyohitajika?** | | |
| **7. Je, mradi ulikamilika ndani ya muda uliowekwa?** | | |
| **8. Je, tathmini ya kukamilisha mradi ilifanyika na cheti kutolewa, ikiwa ilifanyika?** | | |
| **9. Je, wasimamizi wa mradi ni kina nani?** | | |
| **10. Je, wasimamizi wa mradi walihifadhi stakabadhi vizuri?** | | |

| | | |
|---|---|---|
| **11. Je, pesa zilizotengwa kwa ajili ya mradi zilitumika kwa madhumuni ambayo yalikusudiwa?** | | |
| **12. Je, wanajamii wameshiriki vya kutosha katika mradi?** | | |
| **13. Je, wasimamizi wa mradi wameshiriki taarifa muhimu ili kuwezesha umma kufuatilia mradi huo?** | | |
| **14. Je, fedha zimetumika vibaya katika mradi huo?** | | |

**Tembelea learn.tearfund.org/sa-tools ili upakue mwongozo maalum unaoweza kubadilisha kulingana na hali iliyopo.**

# Kiambatisho: Hatua muhimu za mpango wa maendeleo ya serikali

Chati hii inajumuisha nyenzo zinazopatikana katika mwongozo huu, pamoja na maelezo na nyenzo zingine zinazotumika katika mchakato.

| Hatua muhimu za mpango wa maendeleo ya serikali |
|---|
| **Kufuatilia na kuchangia mipango ya kimkakati na kuandaa bajeti** |
| **1.** Mchakato wa mipango shirikishi<br>**2.** Kuchangia kuunda bajeti<br>**3.** Ufuatiliaji wa bajeti<br>**4.** Uandishi wa habari wa raia<br>**5.** Kadi za tathmini ya jamii<br>**6.** Mkataba wa Maelewano (MoU)<br>**7.** Haki ya kupata taarifa (inasaidia nyenzo za ukaguzi wa kijamii kwani inasaidia kuboresha nyenzo zingine)<br>**8.** Stakabadhi za huduma za umma |

| Kufuatilia utekelezaji wa miradi na mipango |
|---|
| 1. Ufuatiliaji wa bajeti<br>2. Uandishi wa habari wa raia<br>3. Kushughulikia malalamishi<br>4. Mkataba wa Maelewano (MoU)<br>5. Uchunguzi wa ufuatiliaji wa matumizi ya umma<br>6. Ukaguzi wa kijamii<br>7. Haki ya kupata taarifa<br>8. Stakabadhi za huduma za umma<br>9. Kandarasi za umma (hutumika wakati mahususi, k.m wakati wa kampeni za uchaguzi) |
| **Kufuatilia matokeo ya maendeleo** |
| 1. Ufuatiliaji wa bajeti<br>2. Uandishi wa habari wa raia<br>3. Kadi za tathmini ya jamii<br>4. Ripoti za umma<br>5. Haki ya kupata taarifa |

# Marejeleo


- Abunada, Mo'min (2015) Manual on Social Accountability for Civil Society Organizations and Municipalities in Palestine
- Tearfund (2008) Accountability – Footsteps 76
- Berthin, G (2011) A Practical Guide to Social Audit as a Participatory Tool to Strengthen Democratic Governance, Transparency and Accountability
- CARE Malawi (2013) The Community Score Card (CSC): A generic guide for implementing CARE's CSC process to improve quality of services
- Chapa, DR et al (1997) Inter-regional project for participatory upland conservation and development – Nepal – Participatory rural appraisal and planning in the Bhusunde Khola watershed from October 1995 to January 1996
- CIVICUS (2015) Participatory Governance Toolkit
- Pekkonen, Anu (2009) Monitoring & Evaluation of Public Services, Tool: Community Score Cards (CIVICUS)
- Escher, Julia (2022) 'Community Score Cards – a powerful tool to improve public services' (Civil Society Academy)
- Rietbergen-McCracken, Jennifer (2010) Participatory Development Planning (CIVICUS)
- County Governance Toolkit (2018) Social Accountability Mechanisms and Tools

- David, Prince (2008) Biblical accountability – Bible study in Accountability – Footsteps 76 (Tearfund)
- Gikonyo, Wanjiru (2008) The CDF Social Audit Guide: A Handbook for Communities (Open Society Initiative of East Africa)
- Grandvoinnet, H., Aslam, G. na Raha, S. (2015).Opening the black box:  The contextual drivers of social accountability.Washington, DC: World Bank Publications.
- Kohli, Divya Singh (2012) Manual on Social Accountability: Concepts and Tools (Centre for Budget and Governance Accountability)
- Kumar, Dinesh and Punam Gupta (2021) 'Communicating in Media Dark Areas' from Effective Strategies for Communicating Insights in Business
- Lawson, Melissa and Joanna Watson (2016) CCM Advocacy Guide:  Jinsi ya kuhusisha utetezi wa mashinani katika uhamasishaji wa kanisa na jamii (Tearfund)
- Mare, Admire et al (2018) Citizen Journalism Guidelines on Electoral Reporting in Zimbabwe (International Media Support)

- McDevitt, Andy (2011) Social Accountability Topic Guide (Transparency International)
- Oduor, Chrispine O (2014) Handbook on County Planning, County Budgeting and Social Accountability (Institute of Economic Affairs, Kenya)
- Kolybashkina, Nina and Mitra Motlagh (2012) Social Accountability in a Changing Region: Actors and Mechanisms (United Nations Development Programme: Regional Bureau for Arab States)
- Tearfund (2016) Monitoring government spending (budget tracking) – a good practice guide from the Reveal toolkit: Corruption and governance
- Xin, Xin (2010) The Impact Of "Citizen Journalism" On Chinese Media And Society from Journalism Practice
- Yuliani, Elizabeth L (2004) 'Decentralization, deconcentration and devolution: what do they mean?' Cifor (Center for International Forestry Research)

**‘Lakini hukumu na iteremke kama maji, na haki kama maji makuu’**

**Amosi 5:24**

**learn.tearfund.org**
+44 (0)20 3906 3906 publications@tearfund.org

Ofisi iliyosajiliwa: Tearfund, 100 Church Road, Teddington, TW11 8QE. Kampuni yenye dhima yenye kikomo kwa dhamana, iliyosajiliwa nchini Uingereza: 994339. Nambari ya Shirika la Hisani Lililosajiliwa 265464 (Uingereza na Wales). Nambari ya Shirika la Hisani Lililosajiliwa SC037624 (Scotland) J1027 – (1023)

tearfund